

**ULINGANISHAJI WA UJIFUNZAJI STADI ZA KISWAHILI KWA
WANAFUNZI WENYE ULEMAVU WA MACHO KATIKA SHULE
JUMUISHI KATIKA KAUNTI ZA NAKURU NA KISUMU, KENYA.**

ABUNGA LILIAN MUGUCHE

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI
YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA.**

JUNI, 2022

IKIRARI

Kazi hii ni yangu mwenyewe na haijatolewa kwa chuo kingine kwa mahitaji ya kuhitimu shahada ya aina yoyote.

Sahihi... Abunga Tarehe... 03/06/2022

Abunga Lilian Muguche

C50/NKU/CE/34302/2017

Tasnifu hii imetolewa kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa ruhusa yangu kama msimamizi.

Prof. Peter Githinji

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu cha Kenyatta

Sahihi... Peter Githinji Tarehe... 03/06/2022

TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa wazazi wangu Jeremiah Abunga na Sairet Moraa kwa kunilea, kunipa nafasi ya kupata elimu na kunipa moyo wa kuendeleza masomo yangu. Vilevile, naitabarukia ndugu zangu Douglas Abunga na Mark Abunga kwa kunitia shime kila wakati. Mmechangia katika ufanisi huu kwa kiasi kikubwa. Mungu awape maisha marefu.

SHUKRANI

Kwanza kabisa namshukuru Maulana kwa mapenzi yake kwangu hadi kuyakamilisha masomo yangu ya uzamili.

Shukrani za dhati kwa msimamizi wangu Prof. Peter Githinji ambaye hakuchoka kusoma kazi yangu na kunitia moyo wa kuendelea bila kutamauka. Asante sana Prof. kwa ushauri na uongozi wako katika kila hatua ya kazi hii. Vilevile, namshukuru Dkt. David Kihara kwa kunishika mkono katika safari hii ya masomo yangu.

Pia nawashukuru wahadhiri wote katika idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta walionifundisha wakiwemo Prof. Wendo Nabea, Dkt. John Oteyo, Dkt. Mayaka Gwachi. Asanteni kwa kunihimiza kulenga juu masomoni na kuhakikisha kuwa nimefaulu.

Mwisho nawashukuru wote waliochangia ufanisi wa utafiti huu wakiongozwa na baadhi ya walimu wa Kiswahili katika shule ya Menengai na Joel Omino kwa kuniruhusu kutangamana na wanafunzi wao na kupata data iliyofanikisha utafiti huu. Shukrani na Mungu awabariki.

IKISIRI

Mawasiliano bora hutegemea uelewa wa stadi za lugha katika lugha husika. Ujifunzaji wa stadi za lugha ni kipengele muhimu katika lugha yoyote na huhusisha kusikiliza, kusoma, kuandika na kuzungumza kwa kiwango kikubwa ili kupata maana iliyokusudiwa katika muktadha husika. Utafiti huu ulilenga kubainisha tofauti za changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi za Menengai na Joel Omino katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Vilevile, kulinganisha tofauti za usuli wa mazingira ya ujifunzaji kati ya shule jumuishi ya Menengai na Joel Omino na kuchambua athari za tofauti za kimazingira kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili. Kazi hii iliongozwa na Nadharia ya Usomi Tendaji ya Bruner (1966). Kulingana na nadharia hii, mchakato wa ujifunzaji huwa bora zaidi wanafunzi wakishirikishwa kwani wao hujenga maana pamoja na hivyo, kuimarishana kiujuzi. Utafiti huu ulifanywa maktabani na nyanjani. Shule jumuishi za msingi zilizotafitiwa ni Menengai na Joel Omino. Sampuli ilituliwa kwa kutumia mbinu ya kimaksudi. Data ilikusanywa kwa kuhoji wanafunzi wote wenye ulemavu wa macho na baadhi ya walimu wa Kiswahili ilhali hojaji zilijazwa na wanafunzi wote wenye ulemavu wa macho na baadhi ya wanafunzi wasio na ulemavu wa macho. Mbinu ya uchunzaji ilitumika pia kuchunguza uhusiano wa mwalimu anapofunza na kuongoza kila shughuli darasani huku mwanafunzi akifuata maagizo na kujifunza. Data iliyokusanywa ilirekodiwa na kuchanganuliwa kwa kuzingatia maswali, malengo na nadharia ya utafiti. Matokeo ya utafiti yalibaini kuwa, kuna changamoto nyingi zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule mbili lengwa. Hata hivyo, kuna changamoto zinazotofautiana katika shule hizi. Matokeo yalithibitisha kuwa, kuna tofauti tano za kimazingira kati ya shule zilizolengwa. Aidha, athari hasi na chanya zilitambulika kutokana na tofauti za kimazingira kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yatawapa walimu wa lugha wanaofunza katika shule jumuishi na wakati mwingine shule maalum uelewa wa mbinu bora za kufunzia wanafunzi wenye ulemavu wa macho stadi za lugha ya Kiswahili. Aidha, matokeo ya utafiti huu pia yatasaidia washikadau katika elimu kama vile; Wizara ya Elimu, Taasisi ya kukuza mitalaa na watafiti wa masuala ya lugha na ulemavu wa macho.

ABSTRACT

Effective communication relies on the comprehension of appropriate skills in the relevant language. Learning language skills is an important aspect in any language and it depends on listening, reading, writing and speaking to a large extent in order to get the intended meaning in the relevant context. This research aimed at determining the differences in the challenges that visually impaired students face in Menengai and Joel Omino integrated primary schools when learning Kiswahili language. Similarly, comparing the differences of the learning environments between Menengai and Joel Omino integrated schools and analysing the effects of different environments on visually impaired students when learning Kiswahili language skills. This research was guided by Active Learning Theory by Bruner (1966). According to this theory, the learning process is effective when students work together since they create new meaning and therefore, enhance their knowledge. The study was done in the library and in the field. The integrated primary schools which were researched on were Menengai and Joel Omino. Samples were obtained by use of purposive sampling method. Data was obtained by interviewing all students with visual impairment and some of the Kiswahili teachers while questionnaires were filled by all students with visual impairment and some students who are not visually impaired. Observation method was also used to investigate the relationship of the teacher when teaching and guiding every activity in the classroom while a student follows the instructions and learns. Data collected was recorded and analyzed in accordance with the research questions, objectives and theory. The results of this research revealed that there are many challenges facing visually impaired students in both schools. However, some challenges vary in these schools. These findings further revealed that there are five environmental differences between the two selected schools. In addition, negative and positive effects were identified on visually impaired students due to environmental differences when learning Kiswahili language skills. The results of this research will give language teachers who teach integrated schools and in some cases special schools knowledge about the effective methods to use when teaching Kiswahili language skills to students with visual impairment. The results of this research will also help education stakeholders such as; The Ministry of Education, curriculum developers and researchers in language and visual impairment.

UFAFANUZI WA ISTILAHU MUHIMU

- Elimu jumuishi:** Mwingiliano wa wanafunzi walio na wasio na ulemavu katika mazingira sawa kielimu.
- Stadi za lugha:** Maarifa au ujuzi unaotumiwa na watu katika kuwasiliana kwa kutumia lugha.
- Shule jumuishi:** Taasisi ambayo wanafunzi walio na ulemavu wa aina fulani hufunzwa pamoja na wanafunzi wasio na ulemavu bila mtalaa kubadilishwa kwa kiwango chochote kikubwa.
- Ulemavu wa macho:** Hali ya kukosa kuona kabisa au kuona kwa shida, hata wakati mtu amevaa lenzi za kurekebisha.

ORODHA YA VIFUPISHO

CRES

Centre for Research Ethics and Safety

NACOSTI

National Commission for Science, Technology & Innovation

YALIYOMO

IKIRARI.....	ii
TABARUKU.....	iii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI.....	v
ABSTRACT.....	vi
UFAFANUZI WA ISTILAH MUHIMU	vii
ORODHA YA VIFUPISHO	viii
ORODHA YA MAJEDWALI	xii
ORODHA YA CHATI	xiii
ORODHA YA GRAFU	xiv
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI.....	1
1.0 Usuli wa Mada	1
1.1 Suala la Utafiti	3
1.2 Malengo ya Utafiti	5
1.3 Maswali ya Utafiti	5
1.4 Sababu za Kuchagua Mada.....	5
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti.....	7
1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada	8
1.6.1 Tafiti za Kijumla Kuhusu Ujifunzaji wa Lugha.....	8
1.6.2 Tafiti Kuhusu Mazingira ya Ujifunzaji	11
1.6.3 Tafiti Bayana Kuhusu Stadi za Lugha ya Kiswahili	13
1.7 Misingi ya Kinadharia	14
1.7.1 Mihimili ya Nadharia ya Usomi Tendaji	15
1.8 Mbinu za Utafiti.....	17
1.8.1 Muundo wa Utafiti	17
1.8.2 Eneo la Utafiti	17
1.8.3 Uteuzi wa Sampuli	17
1.8.4 Mbinu za Ukusanyaji Data.....	19
1.8.5 Maadili ya Utafiti	20
1.8.6 Uchanganuzi wa Data	21
1.8.7 Uwasilishaji wa Matokeo	21

1.9 Hitimisho	21
SURA YA PILI: TOFAUTI ZA CHANGAMOTO ZINAZOWAKUMBA	
WANAFUNZI WENYE ULEMAVU WA MACHO KATIKA	
SHULE JUMUISHI KATIKA UJIFUNZAJI WA LUGHA YA	
KISWAHILI	22
2.0 Utangulizi.....	22
2.1 Changamoto Zinazotokana na Mazingira ya Darasani	23
2.1.1 Muda wa Ufunzaji na Ujifunzaji.....	23
2.1.2 Ukosefu wa Ujuzi wa Walimu	26
2.1.3 Idadi Kubwa ya Wanafunzi Madarasani	27
2.1.4 Mtazamo Hasi wa Walimu na Wanafunzi	30
2.1.5 Ukosefu wa Vitabu Vifaavyo na Vifaa vya Ufunzaji na Ujifunzaji	31
2.1.6 Idadi Ndogo ya Walimu Wanaofunza Somo la Kiswahili	34
2.1.7 Kutegemea Wanafunzi Wasio na Ulemavu wa Macho.....	35
2.2 Changamoto Zinazotokana na Mazingira ya Nyumbani	37
2.2.1 Ushirikiano Kutoka kwa Wazazi	37
2.2.2 Hali ya Umaskini.....	39
2.3 Changamoto Zinazotokana na Mazingira ya Shuleni	41
2.3.1 Maeneo ambapo Shule Inapatikana	41
SURA YA TATU: TOFAUTI ZA USULI WA MAZINGIRA YA UJIFUNZAJI	
KATI YA SHULE JUMUISHI YA MENENGAI NA JOEL	
OMINO	44
3.0 Utangulizi.....	44
3.1 Tofauti ya Walimu wa Kiswahili kati ya Shule Mbili Lengwa	45
3.2 Tofauti ya Ushirikiano wa Wazazi kati ya Shule ya Menengai na Joel Omino	46
3.3 Tofauti ya Tajiriba ya Walimu kati ya Shule Jumuishi Lengwa	48
3.4 Tofauti ya Upatikanaji wa Chumba Maalum katika Shule Lengwa	51
3.5 Tofauti ya Usuli wa Lugha kati ya Shule ya Menengai na Joel Omino	54
3.6 Hitimisho.....	57

SURA YA NNE: ATHARI ZA TOFAUTI ZA KIMAZINGIRA KWA	
WANAFUNZI WENYE ULEMAVU WA MACHO KATIKA	
UJIFUNZAJI WA STADI ZA LUGHA YA KISWAHILI.....	58
4.0 Utangulizi.....	58
4.1 Athari ya Mazingira ya Kelele.....	58
4.2 Athari inayotokana na Hali ya Kiuchumi	62
4.3 Athari ya Usuli wa Lugha.....	65
4.3.1 Uambishaji na Ngeli.....	66
4.3.2 Idadi ya Fonimu	68
4.3.3 Mofolojia.....	69
4.3.4 Sintaksia	70
4.4 Athari ya Tajiriba ya Kufunza	72
4.5 Athari inayotokana na Mielekeo ya Watu	74
4.6 Athari ya Idadi ya Walimu na Wanafunzi	76
4.7 Hitimisho	80
SURA YA TANO: MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA	
UTAFITI	82
5.0 Utangulizi.....	82
5.1 Muhtasari wa Utafiti	82
5.2 Matokeo ya Utafiti	83
5.3 Mapendekezo Kutokana na Utafiti	86
5.4 Mapendekezo Kuhusu Tafiti za Baadaye	87
Marejeleo.....	89
VIAMBATISHO.....	97
Kiambatisho A: Maswali ya Mahojiano kwa Walimu wa Kiswahili	97
Kiambatisho B: Maswali ya Mahojiano kwa Wanafunzi Walio na Ulemavu wa	
Macho	99
Kiambatisho C: Maswali ya Hojaji kwa Wanafunzi Walio na Wasio na Ulemavu wa	
Macho	100
Kiambatisho D: Vibali vya Kufanya Utafiti.....	103

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1.1: Idadi ya Wanafunzi Walio na Ulemavu wa Macho katika Shule Jumuishi ya Menengai na Joel Omino	18
Jedwali 2.1: Idadi ya Wanafunzi katika Shule Jumuishi za Menengai na Joel Omino	28
Jedwali 2.2: Idadi ya Walimu na Wanafunzi katika kila darasa la Shule ya Joel Omino na Menengai	34
Jedwali 2.3: Ulinganishaji wa Chagamoto Zinazowakumba Wanafunzi wenye Ulemavu wa Macho katika Shule Lengwa.....	42

ORODHA YA CHATI

Chati 3.1: Lugha za Asili za Wanafunzi wa Shule ya Menengai	54
Chati 3.2: Lugha za Asili za Wanafunzi wa Shule ya Joel Omino.....	56

ORODHA YA GRAFU

Grafu 3.1: Tajiriba ya Ufunzaji katika Shule ya Menengai.....	49
Grafu 3.2: Tajiriba ya Ufunzaji katika Shule ya Joel Omino	50

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.0 Usuli wa Mada

Gompel na wenzake (2004) wanasema kuwa, uwezo wa kuona ni mojawapo ya mambo mengi yanayoathiri uwezo wa kukuza ustadi wa kusoma na hivyo kuathiri matokeo katika masomo. Wanaendelea kusema kuwa, watoto walio na uwezo wa chini wa kuona huwa na pembejeo zilizoharibika za kuona na mara nyingi wanahitaji muda na juhudi zaidi kwa utambuzi wa maneno wakati wa kusoma. Kutokana na hayo, uwezo mdogo wa michakato ya kiakili hubaki ili kuelewa maandishi. Basaran (2012) naye anasema kuwa, jinsi wanafunzi wenye ulemavu wa macho wanatambua ulimwengu na shughuli za darasani ni tofauti na wale wasio na ulemavu wa macho. Agesa (2014) anasema kuwa kimsingi, wanafunzi wenye ulemavu wa macho huwa na ugumu wa kusoma lugha ya pili kwani uwezo wa kuona huwa na kazi muhimu katika kujifunza lugha.

Ulemavu wa macho unarejelea upungufu wa uwezo wa kuona hata wakati mtu binafsi amevaa lenzi za kurekebisha (Agesa, 2014). Keefe (1994) anasema kuwa ulemavu wa macho husababishwa na magonjwa ya macho, ajali au hali aliyozaliwa nayo mtu. Kwa mujibu wa Arslantas (2017) ulemavu wa macho umegawanywa katika kategoria nne ambazo ni; upungufu wa uwezo wa kuona, uwezo wa chini wa kuona, upofu unaokubalika kisheria na upofu kamili. Kulingana naye, upungufu wa uwezo wa kuona hurejelea aina fulani ya shida ya kuona ambayo si ya hali ya juu, hata hivyo, watu walio na upungufu wa kuona huhitaji msaada zaidi katika masomo yao. Watu

walio na uwezo wa chini wa kuona wana ulemavu wa macho wa hali ya juu kwani hawana uwezo wa kusoma maandishi ya kawaida ambayo hayawezi kuboreshwa kwa miwani ya kawaida. Upofu unaokubalika kisheria ni istilahi inayorejelea kiwango cha upungufu wa uwezo wa kuona ambao umekubalika kisheria ili kuamua ustahiki wa faida. Upofu kamili unarejelea watu wasioona kitu chochote kwa kutumia macho yao kwani hawawezi kuona aina yoyote ya mwanga.

Katika kujifunza lugha ili kuitumia kama njia ya mawasiliano, wanafunzi wanahitaji kushughulikia stadi nne kuu ambazo ni; kuongea, kusikiliza, kuandika na kusoma. Kila stadi humwezesha mwanafunzi kutumia stadi zingine na pia kudhibiti vipengele vingine muhimu katika ujifunzaji wa lugha. Kusikiliza watu wengine wakitumia lugha humwezesha mtoto kuwa na uwezo wa kuongea. Stadi ya kusoma huwasaidia wanafunzi kukuza uwezo wa kuwasiliana kupitia maandishi (Kurniasih, 2011). Kwa elimu ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho, shule husisitiza kusoma kwa kutumia vitabu vyenye maandishi makubwa na vitabu vilivyochapishwa kwa breli (Nolan na Morris, 1973). Hata hivyo, kulingana nao, wanafunzi wenye ulemavu wa macho hutumia wakati mwingi kusoma vitabu hivi. Wanaendelea kusema kuwa, ujifunzaji wa fasihi kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho huwa bora zaidi wanaposoma kwa kutumia stadi ya kusikiliza kuliko stadi ya kusoma. Hata hivyo, kudumisha umakini wanapotumia stadi ya kusikiliza huwa changamoto kubwa.

Mtafiti alibaini kuwa kuna mambo mengi ambayo huathiri ujifunzaji wa lugha kama vile pembejeo, walimu wa lugha, nyenzo zinazotumika, mielekeo ya wadau mbalimbali, hulka za wanafunzi na pia mazingira. Tunapozingatia mazingira

tunafikiria kuhusu mazingira ambamo shule hupatikana ambayo huathiri sana mazingira ya darasani. Vilevile, suala la mazingira linategemea usuli wa wanafunzi wanaosoma katika shule husika. Kwa kuzingatia umuhimu wa mazingira katika ujifunzaji wa lugha, uchunguzi wa tofauti za changamoto zinazowakumba wanafunzi walio na ulemavu wa macho na athari za tofauti za kimazingira katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule jumuishi ni muhimu kufanywa.

Aidha, ulinganishaji wa tofauti za usuli wa mazingira ya ujifunzaji kati ya shule jumuishi ya Menengai na Joel Omino ulitoa mwanga katika ujifunzaji wa lugha kwani, shule ya Menengai iko katika mji wa Nakuru na wanafunzi wanatoka katika mitaa ambayo wakazi huzungumza lugha tofauti. Vilevile, kuna lugha nyingi ambazo huzungumzwa katika mji wa Nakuru, jambo ambalo hufanya Kiswahili kitumike zaidi. Kwa upande mwingine, shule ya Joel Omino iko Kisumu na ingawa pia Kisumu ni mji, demografia yake ni tofauti. Tofauti na Nakuru, lugha zinazozungumzwa zaidi ni Dholuo, Ekegusii na kwa kiwango fulani Kiluhya. Hivyo basi, utafiti uliotekelezwa ulijikita katika ulinganishaji wa ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule jumuishi katika Kaunti za Nakuru na Kisumu, Kenya.

1.1 Suala la Utafiti

Ujifunzaji wa lugha yoyote ile hutegemea stadi za uandishi, usomaji, uzungumzaji na usikilizaji. Stadi za uandishi na usomaji bila shaka huwa na changamoto kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho. Wanafunzi walio na ulemavu wa macho

hupata changamoto wanapojifunza stadi za lugha kwani wanahitaji muda na juhudi zaidi wakati wa kusoma na kuandika ikilinganishwa na wanafunzi wasio na ulemavu wa macho. Licha ya haya, tafiti nyingi za awali zilizoshughulikia ujumuishaji zilizingatia elimu kwa jumla ilhali utafiti huu ulizingatia lugha ya Kiswahili. Aidha, tafiti zilizofanywa kuhusu masuala ya lugha kwa wanafunzi wenye ulemavu zilizingatia zaidi elimu maalum badala ya ujumuishaji. Ili kupata picha kamili ya masuala mbalimbali ambayo huwakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa lugha, kuna umuhimu wa kubainisha tofauti za changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi.

Utafiti huu ulilenga shule jumuishi za msingi za Menengai na Joel Omino katika kulinganisha tofauti za usuli wa mazingira na vilevile, kuchambua athari za tofauti hizo kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa stadi za Kiswahili. Katika mazingira ya wingi lugha kama vile Nakuru, kuna lugha mseto ambapo usuli na pembejeo za lugha ni tofauti ikilinganishwa na mazingira ambayo kwa kiasi kikubwa ni ya lugha moja kama vile shule iliyoko katika mji wa Kisumu. Kupitia ulinganishaji, tutaweza kuelewa ni stadi zipi za lugha ambazo huathiriwa zaidi na tofauti za mazingira ya ujifunzaji katika juhudi za kuimarisha ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho.

1.2 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga:

1. Kubainisha tofauti za changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi za Menengai na Joel Omino katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.
2. Kulinganisha tofauti za usuli wa mazingira ya ujifunzaji kati ya shule jumuishi za Menengai na Joel Omino.
3. Kuchambua athari za tofauti za kimazingira kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili.

1.3 Maswali ya Utafiti

Maswali yaliyojibiwa na utafiti huu ni:

1. Je, kuna tofauti zipi za changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi za Menengai na Joel Omino katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.?
2. Tofauti za usuli wa mazingira ya ujifunzaji zinalingana kwa namna gani kati ya shule jumuishi za Menengai na Joel Omino?
3. Tofauti za kimazingira huwa na athari gani kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili?

1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Lugha ya Kiswahili imekuwa lugha muhimu nchini na katika jumuiya ya Afrika Mashariki na hivyo basi, imekuwa muhimu kuwapa Wakenya wote maarifa sawa katika lugha ya taifa na rasmi ili waweze kutekeleza wajibu wao kama wananchi katika taifa. Ili kushughulikia masuala ya kielimu ya wanafunzi wenye ulemavu wa

macho, wanafunzi hawa wanaweza kuwa katika shule maalum au shule jumuishi. Shule maalum kwa kawaida huwa na wale ambao hawana uwezo wa kuona kabisa ilhali shule jumuishi, ingawa hushughulikia wale wenye uwezo wa chini wa kuona pia huwa na wanafunzi wasiiona hata kidogo. Kwa wanafunzi wowote wale, ujifunzaji wa lugha huwa msingi wa ufanisi katika elimu na pia katika maisha kwani lugha huwa kiungo muhimu kazini na katika utangamano wa wanajamii. Kutokana na hayo, kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anapata maarifa bora wakati wa kujifunza lugha. Hivyo basi, kuna haja ya kuchunguza jinsi wanafunzi wenye ulemavu wa macho wanajifunza lugha hii.

Mada hii ilitokana na kutambua kuwa kuna utagusano wa mazingira na ujifunzaji wa lugha ya pili. Tafiti nyingi za awali zilizoshughulikia ujumuishaji kama vile (Mwakyeya, 2013 na Otyola na wenzake, 2017) zilizingatia elimu kwa jumla, ilhali huu ulizingatia lugha ya Kiswahili. Zile zilizoshughulikia masuala ya lugha kwa wanafunzi wenye ulemavu kama vile (Arslantas, 2017 na Basaran, 2012) zilizingatia zaidi elimu maalum badala ya ujumuishaji. Pili, mada hii ilitokana na kutambua kuwa lugha ya Kiswahili ina upekee wake kwani ni lugha ambishi bainishi ambapo mzizi lazima ujumlishe viambishi mbalimbali ambavyo hubeba vipengele vya kisarufi, jambo ambalo humbidi mwanafunzi afafanue neno, maana ya neno na pia sarufi. Hii hufanya lugha ya Kiswahili kuwa na changamoto fulani ambazo hazimo katika lugha zingine kama vile Kiingereza.

Mwishowe, kuwa na ulemavu wa macho humfanya mwanafunzi kuchukua muda mwingi kusoma na kuandika ikilinganishwa na wanafunzi wasio na ulemavu wa

macho wanaosoma nao katika darasa moja. Mwanafunzi asiposoma sana, kiwango chake cha kumudu sarufi, msamiati, nahau, methali na vipengele vingine muhimu katika lugha huathirika. Kila eneo, kila shule na kila mwanafunzi huwa na upekee wake katika ujifunzaji wa lugha, upekee ambao hujengwa na uhalisia unaowazunguka wadau wote katika ujifunzaji wa lugha kwa jumla. Katika kuhakikisha kuwa kila kipengele katika ujifunzaji wa Kiswahili kinashughulikiwa, utafiti huu unanuia kuchangia katika kufafanua jinsi tofauti za kimazingira zinaweza kuathiri uimarishaji wa stadi za lugha ya Kiswahili.

1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulilinganisha ujifunzaji wa stadi za Kiswahili kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule jumuishi katika Kaunti za Nakuru na Kisumu, Kenya. Katika kuangazia mazingira ya darasani, baadhi ya wanafunzi wasio na ulemavu wa macho katika shule hizi mbili pia walihusishwa. Utafiti huu ulizingatia darasa la nne hadi la saba peke yake. Madarasa hayo manne yalichaguliwa kwani wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika madarasa hayo wanahitajika kuwa wameimarika katika ujuzi wa stadi za lugha ya Kiswahili.

Mtafiti alizingatia madarasa ambayo yana wanafunzi wenye ulemavu wa macho tu. Jinsia zote mbili za wanafunzi zilihusishwa katika madarasa hayo manne. Walimu wa Kiswahili peke yao ndio waliohojiwa na si wa masomo mengine. Kutokana na uhaba wa shule jumuishi, shule mbili zilihusishwa; moja katika Kaunti ya Nakuru na nyingine katika Kaunti ya Kisumu, Kenya. Mtafiti alichunguza mazingira ya darasani (wanafunzi wenye ulemavu wa macho na wasio na ulemavu wa macho), mazingira ya

shuleni yaani, eneo ambalo shule inapatikana (mji wenye wingi lugha na mji ambao kwa kiasi kikubwa ni lugha moja inayotumika) na mazingira ya nyumbani.

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Sehemu hii imegawanywa katika vijisehemu vitatu ambavyo ni; tafiti za kijumla kuhusu ujifunzaji wa lugha, tafiti kuhusu mazingira ya ujifunzaji na tafiti bayana kuhusu stadi za lugha ya Kiswahili.

1.6.1 Tafiti za Kijumla Kuhusu Ujifunzaji wa Lugha

Arslantas (2017) akichunguza kuhusu ujifunzaji wa lugha ya kigeni kwa watu wenye ulemavu wa macho, anasema kuwa katika mazingira yoyote ya kielimu, stadi nzuri ya kusikiliza huwasaidia wanafunzi wenye ulemavu wa macho kufanikiwa katika stadi ya kusoma na pia kuwasiliana kupitia maandishi na kuzungumza. Anaongeza kuwa stadi ya kusikiliza imebainika kuwa bora zaidi kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho ikilinganishwa na stadi ya kusoma. Vilevile, anasema kuwa wakati mahitaji maalum ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho yameshughulikiwa, wanaweza kujifunza lugha yoyote ya kigeni kama wanafunzi wenzao walio na uwezo wa kuona. Licha ya kuwa Arslantas (2017) ameshughulikia ujifunzaji wa lugha kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho, utafiti wake haukushughulikia mazingira ya shule jumuishi. Utafiti huu wa sasa ulikusudia kulijaza pengo hilo.

Akichunguza ufunzaji wa stadi nne za lugha katika madarasa ya chuo kikuu, Aydoğan (2014) anaeleza kuwa stadi ya uandishi ndiyo inayotumika sana ikilinganishwa na stadi hizo zingine tatu za lugha. Anaendelea kusema kuwa walimu wanafaa

wawahimiza wanafunzi wajitegemee, hivyo basi, stadi za lugha zinafaa zifunzwe katika kila darasa. Anapendekeza kuwa walimu wanapofunza stadi nne za lugha wanafaa waunde vifaa na mada zinazokidhi mahitaji na maslahi ya wanafunzi. Utafiti wa Aydoğan (2014) ingawa umejishughulisha na ufunzaji wa stadi za lugha, ulishughulikia wanafunzi wasio na ulemavu wa macho katika chuo kikuu ilhali utafiti huu ulishughulikia wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule jumuishi za msingi. Hata hivyo, utafiti wa Aydoğan (keshatajwa) ulitoa mwanga kwa utafiti wa sasa kwani ulisaidia mtafiti kuelewa zaidi kuhusu stadi nne za lugha.

Susanto na Nanda (2018) walichunguza ufunzaji na ujifunzaji wa Kiingereza kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule maalum, wanasema kuwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho hupata changamoto wanapojifunza lugha kwani vifaa vya kufundishia vinavyotumika mara nyingi huwa vya wanafunzi wasio na ulemavu wa macho. Wanaendelea kusema kuwa changamoto nyingine ni kuwa, walimu hawaelewi mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho na hivyo basi, hawajui kuwashughulikia wanafunzi hao. Utafiti wa Susanto na Nanda (2018) unatofautiana na utafiti uliotekelezwa kwa kuwa hawakushughulikia ujifunzaji wa stadi za lugha, kipengele ambacho utafiti wa hivi sasa ulishughulikia. Aidha, utafiti wao unajikita katika mazingira ya shule maalum.

Mwakyeya (2013) akitafiti kuhusu ufundishaji wa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika madarasa jumuishi, alibaini kuwa walimu wengi hawana ujuzi wa kutosha kuhusu elimu jumuishi. Anaendelea kusema kuwa, serikali inafaa kuboresha hali ilivyo ya elimu jumuishi kwa kuwapa walimu mafunzo yanayofaa katika elimu

maalum ili waweze kufunza ifaavyo. Katika utafiti huu alipendekeza kuwa serikali inafaa pia kuzipa shule fedha za kutosha ili kuhakikisha kuwa vifaa vya kufundishia vinapatikana na hivyo basi, kufanikisha ujifunzaji bora kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika madarasa jumuishi. Utafiti wa sasa ulikuza utafiti wa Mwakyeja (2013) kwa kulinganisha ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule jumuishi katika Kaunti za Nakuru na Kisumu. Katika utafiti huu, Mwakyeja (2013) alichunguza jinsi walimu wanavyowafundisha wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika madarasa jumuishi na shida walimu hao wanazozipitia ambayo ni kinyume na utafiti wa sasa ulioshughulikia tofauti za changamoto ambazo zinawakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi za Menengai na Joel Omino katika kuimarisha stadi za lugha ya Kiswahili. Vilevile, Mwakyeja (2013) alishughulikia ufunzaji kwa jumla kwa wanafunzi wa shule ya sekondari ilhali utafiti huu ulilenga kulinganisha mazingira ya ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili.

Basaran (2012) akichunguza ufunzaji wa Kiingereza kama lugha ya pili kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule maalum, alibaini kuwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho hutambua ulimwengu wao kwa namna iliyo tofauti na wenzao wasio na ulemavu wa macho. Anaendelea kusema kuwa, walimu wa Kiingereza walitumia vifaa na mbinu zilezile za ufunzaji ambazo hutumiwa kwa wanafunzi wasio na ulemavu wa macho. Utafiti wa Basaran (2012) unatofautiana na huu kwani ingawa ameshughulikia ufunzaji wa lugha, amejishughulisha na lugha ya Kiingereza. Vilevile, utafiti huo umefanywa katika shule maalum ya chekechea.

Kulingana na Otyola na wenzake (2017), ujumuishaji wa wanafunzi walio na ulemavu wa macho na wasio na ulemavu wa macho una manufaa si kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho tu bali pia kwa wasio na ulemavu wa macho kwani unaboresha utangamanaji katika jamii. Wanadai kuwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho hupitia changamoto nyingi katika mazingira ya shule jumuishi kwani wao huandika polepole ikilinganishwa na wanafunzi wasio na ulemavu wa macho. Vilevile, wao huwa na maendelezo mabaya ya maneno kwani hawawezi kuona vizuri jinsi maneno yameendelezwa ubaoni. Wakichunguza changamoto zinazowakabili wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika chuo kikuu, Otyola na wenzake (keshatajwa) walibaini kuwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho hawapewi muda wa kutosha wanapokuwa wakifanya mitihani yao. Utafiti wa Otyola na wenzake (2017) ulifaidi utafiti huu kwa kuwa huu pia ulilenga kubainisha tofauti za changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi. Utafiti huu unatofautiana na wa sasa kwani huu ulifanywa katika chuo kikuu ambacho hakina changamoto zilizoko katika shule ya msingi. Aidha, utafiti huu haukushughulikia ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili ambao utafiti wa sasa ulikusudia kuchunguza.

1.6.2 Tafiti Kuhusu Mazingira ya Ujifunzaji

Utafiti wa Kiatkheeree (2018) ulichunguza mazingira ya ujifunzaji kwa upataji wa lugha ya pili. Anasema kuwa mazingira ya ujifunzaji yana athari kubwa kwa kiwango cha ustadi wa lugha ambacho mwanafunzi atakua nacho. Anatoa mfano wa utagusano wa mwanafunzi na mwalimu kama sehemu ya mazingira ya ujifunzaji, inachukuliwa kama jambo muhimu katika kukuza ufanisi wa mwanafunzi. Anapendekeza kuwa

shule zinafaa kuwapa wanafunzi madarasa yaliyo bora, walimu pia wapewe msaada wanaohitaji ili wawape wanafunzi mafunzo yaliyo na ubora na vilevile, shule zito vifaa vinavyotumika wakati wa kujifunza ili kujenga mazingira bora ya ujifunzaji. Utafiti wa sasa ulikuza utafiti wa Kiatkheeree (2018) kwa kulinganisha ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule jumuishi katika Kaunti za Nakuru na Kisumu. Katika utafiti huu, Kiatkheeree (2018) alijikita katika ujifunzaji wa Kiingereza katika mazingira ya shule ya kawaida ambao ni kinyume na utafiti wa sasa uliokusudia kulinganisha ujifunzaji wa Kiswahili katika mazingira ya shule jumuishi.

Wakichunguza uhusiano wa mazingira ya shule na ujifunzaji wa lugha ya Kiingereza, Lodhi na wenzake (2019) walitambua kuwa ufanisi wa kimasomo kwa wanafunzi wa lugha haategemei kiwango chao cha kiakili tu bali pia unahusishwa na mazingira ya ujifunzaji ambayo wamepewa. Wanaendelea kusema kuwa mazingira yana athari chanya au hasi kwa utendaji wa mwanafunzi. Mambo ya kimazingira kama vile, eneo la shule, idadi ya madarasa na walimu, ujuzi na kiwango cha elimu cha mwalimu, uhusiano wa mwalimu na mwanafunzi na vifaa vinginevyo vinavyohitajika katika kufunza na kujifunza huwa na athari ya moja kwa moja katika ujifunzaji wa mwanafunzi. Wanapendekeza kuwa walimu wanapaswa kurekebisha mbinu zao za kufundishia kulingana na mahitaji ya wanafunzi na vilevile wanafaa kuelewa mazingira ya wanafunzi wao. Utafiti wa Lodhi na wenzake (2019) ingawa umejishughulisha na mazingira ya ujifunzaji wa lugha, haukulinganisha mazingira ya ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili katika shule jumuishi.

1.6.3 Tafiti Bayana Kuhusu Stadi za Lugha ya Kiswahili

Utafiti wa Lichuma (2018) ulichunguza mikakati ya kufundishia stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi katika shule za msingi. Anahoji kuwa, walimu wengi hawazingatii mikakati bora ya kufundishia stadi ya kusoma. Anaendelea kusema kuwa, mielekeo na ujuzi wa mwalimu kuhusu jinsi ya kufundishia stadi zote za lugha ina nafasi kubwa katika ufundishaji wa stadi ya kusoma. Alisisitiza kuwa, walimu wahakikishe kuwa wamewafundisha wanafunzi stadi ya kusoma kwa kutumia vitabu vya hadithi vya Kiswahili wakati mwingi. Anaendelea kusema kuwa, walimu wanafaa kujenga mielekeo chanya kuhusu ufunzaji wa stadi ya kusoma ambayo ni muhimu katika mawasiliano na maingiliano ya kijamii. Ijapokuwa Lichuma (2018) alishughulikia ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili katika shule za msingi, alishughulikia wanafunzi wasio na ulemavu wa macho katika shule za kawaida.

Masuala kadha wa kadha kuhusu vipengele tofauti vya lugha kama vile ufahamu, fasihi na isimu jamii yameshughulikiwa. Aidha, mtafiti alisoma kazi nyingi lakini hakukutana na mada ya ujifunzaji wa stadi za Kiswahili katika shule jumuishi ya msingi. Vilevile, kazi nyingi kuhusu ujifunzaji wa lugha zimefanywa katika lugha ya Kiingereza na si lugha za Kiafrika kama vile Kiswahili. Tafiti nyingi kuhusu ujifunzaji wa lugha hufanywa katika shule za kawaida na kwa kiwango fulani shule maalum. Hivyo basi, kuna haja kubwa ya kuendelea kufanya uchunguzi katika shule jumuishi ili kukuza maarifa ambayo yatachangia pakubwa katika kuwapa wanafunzi walio na ulemavu elimu wanayostahili, hasa kwenye masomo ya lugha kama Kiswahili.

1.7 Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Usomi Tendaji iliyoasisiwa na kusukwa kimfumo na Bruner (1966). Dhana muhimu katika Usomi Tendaji ni kuwa, mchakato wa ujifunzaji huwa bora zaidi wanafunzi wakishirikishwa kwani wao hujenga maana pamoja na hivyo, kuimarishana kiujuzi. Nadharia ya Usomi Tendaji imetumiwa na Melly (2019) anayesema kuwa, shughuli ya ufundishaji na ujifunzaji ni shughuli hai inayohitaji mwanafunzi ashirikishwe katika hatua zote za ujifunzaji.

Kwa msingi wa mawazo ya Bruner (1966), Usomi Tendaji huhusisha shughuli za kimwili na kiakili. Shughuli za kimwili zinahitajika ili wanafunzi wawe na uzoefu na vitu katika mazingira yao. Shughuli za kiakili nazo zinahitajika katika ujifunzaji ili kugeuza uzoefu huo kuwa ujuzi. Hivyo basi, elimu ni mchakato wa kubadilisha uzoefu wa kibinafsi. Harris na Graham (1996), wanadai kuwa Usomi Tendaji ni kipengele muhimu kwani huwasaidia wanafunzi kuhifadhi wanachosoma. Walimu huweka msingi wa mafunzo yao katika kile ambacho wanafunzi wanajua tayari ambapo kabla mwalimu aanze kufunza dhana mpya anafaa kujadili dhana zinazohusiana na dhana hizo mpya (Duhaney na Duhaney, 2000). Mwalimu huzingatia mbinu ya kuuliza maswali na kuwapa changamoto wanafunzi watumie ujuzi wao kulijibu swali (Schunk, 2008).

Nadharia hii ni mwafaka katika utafiti huu kwani inadokeza kuwa kila mtu ni mshiriki katika mchakato wa kuunda maana, hivyo basi, ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili unafaa kuonekana kama maafikiano ya kijamii. Kwa hivyo, kazi ambayo wanafunzi walio na ulemavu wa macho wanashirikiana kwa pamoja na wale wasio na

ulemavu wa macho katika shule jumuishi kujifunza stadi za lugha ina misingi yake katika nadharia ya Usomi Tendaji.

1.7.1 Mihimili ya Nadharia ya Usomi Tendaji

Nadharia hii ina mihimili minne. Mhimili wa kwanza ni kuwa, wanafunzi huunda maana yao wenyewe. Kwa hivyo, kujifunza lazima kuanze na masuala yanayopatikana katika mazingira ya wanafunzi wanayotaribu kikamilifu kuunda maana. Walimu wanafaa kutengeneza mazingira bora yatakayotumiwa katika ujifunzaji wa wanafunzi kama vile, kuwahusisha kwa kuwauliza maswali. Mhimili huu ulifaa utafiti huu katika kulinganisha tofauti za usuli wa mazingira ya ujifunzaji kati ya shule jumuishi ya Menengai na Joel Omino. Aidha, ulitumiwa katika kuchambua athari za tofauti za kimazingira kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili.

Pili, ili ufundishaji na ujifunzaji uwe na ubora, maandalizi yanafaa kufanywa kabla ya kuwasilisha somo. Mhimili wa nadharia hii unashikilia kuwa, mwanafunzi anafaa kushirikishwa katika kila hatua ya ujifundishaji na wala si tu kumwekea dhana akilini mwake. Mwalimu anafaa ahakikishe kuwa wanafunzi wanapata hamu ya kujifunza dhana tofauti kwa kutumia vifaa vya ujifunzaji. Mhimili huu ulitumiwa katika utafiti huu kubainisha tofauti za changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi za Menengai na Joel Omino katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

Tatu, ili ujifunzaji uwe bora, lazima mwalimu atambue yale ambayo wanafunzi wanajua na kuwasaidia kuunda mawazo mapya kutokana na msingi huo. Hivyo basi, kabla ya mwalimu kufunza dhana mpya anafaa kuanza na mambo ambayo wanafunzi wanafahamu akielekea kwa wasiyoyaelewa. Mwalimu anafaa awape changamoto wanafunzi wajenge mawazo kutokana na maarifa ya awali na anafaa pia kuelewa changamoto zao kutokana na hali yao. Mhimili huu haukutumika katika utafiti huu kwa sababu haukuingiliana na malengo yaliyokusudiwa kufikiwa na hivyo, haungetusaidia katika uchanganuzi wa data.

Nne, watu huweza kujifunza zaidi wakati wanajifunza na watu wengine kuliko wakati wanajifunza peke yao. Mchakato wa ujifunzaji huwa bora zaidi wanafunzi wakishirikishwa kwani wao hujenga maana pamoja na hivyo basi, kuimarishana kiujuzi. Majadiliano darasani katika vikundi vidogo vidogo huwa muhimu. Mhimili huu hasa ulionyesha umuhimu wa ujumuishaji wa wanafunzi walio na ulemavu wa macho kwani watapata msaada kutoka kwa wenzao wasio na ulemavu wa macho, kuliko wakati wanajisomea peke yao. Hii huwa mojawapo ya mantiki ya kuwa na elimu jumuishi. Mhimili huu ulitusaidia kubainisha tofauti za changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi za Menengai na Joel Omino katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili na vilevile, kulinganisha tofauti za usuli wa mazingira ya ujifunzaji kati ya shule jumuishi ya Menengai na Joel Omino.

1.8 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii inajumlisha mbinu zilizozingatiwa katika uchunguzi huu. Hasa imefafanua muundo na eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, maadili ya utafiti, uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeo na hatimaye hitimisho.

1.8.1 Muundo wa Utafiti

Mtafiti alitumia muundo wa kimaelezo. Muundo huu ulitumika kulinganisha ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule jumuishi katika Kaunti za Nakuru na Kisumu nchini Kenya. Kupitia muundo wa kimaelezo, maelezo kuhusu ulinganifu wa mazingira ya ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kati ya shule jumuishi ya Menengai na Joel Omino yaliwasilishwa.

1.8.2 Eneo la Utafiti

Uchunguzi ulifanyika nyanjani na maktabani. Maktabani mtafiti alisoma maandishi kuhusu mada ili kupata mwelekeo mwafaka. Utafiti wa nyanjani ulifanywa katika shule jumuishi ya msingi ya Menengai na Joel Omino ambapo walimu na wanafunzi wenye ulemavu wa macho walihojiwa. Shule hizi zinapatikana katika Kaunti ya Nakuru na Kaunti ya Kisumu mtawaliwa. Shule hizi mbili ni mwafaka katika utafiti huu kwani zina sifa zinazotakikana kama vile idadi ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Aidha, shule hizi zina historia ndefu ya ujumuishaji wa wanafunzi walio na mahitaji maalum wakiwemo wenye ulemavu wa macho.

1.8.3 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli ya kimaksudi ilitumika kuteua shule jumuishi ya msingi ya Menengai na Joel Omino. Sampuli ya kimaksudi ilitumika kupata idadi ya walimu na wanafunzi

watakaotumika kupata data ya utafiti huu. Kutokana na idadi ndogo ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho, wanafunzi wote tisa kutoka darasa la nne hadi la saba peke yao ndio walilengwa katika shule jumuishi ya Menengai ilhali wanafunzi wanane walilengwa kutoka darasa la nne hadi la saba katika shule jumuishi ya Joel Omino kama inavyodhihirishwa katika jedwali 1.1:

Jedwali 1.1: Idadi ya Wanafunzi Walio na Ulemavu wa Macho katika Shule

Jumuishi ya Menengai na Joel Omino

Shule Jumuishi ya Menengai			Shule Jumuishi ya Joel Omino		
Darasa la	Jinsia		Darasa la	Jinsia	
	Kike	Kiume		Kike	Kiume
Nne	1	2	Nne		1
Tano	2	1	Tano	1	1
Sita	1		Sita	2	1
Saba	2		Saba	2	
Jumla	6	3	Jumla	5	3
9			8		

Madarasa hayo manne yalichaguliwa kwani wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika madarasa hayo wanahitajika kuwa wameimarika katika ujuzi wa stadi za lugha ya Kiswahili. Aidha, wanafunzi hao wamekuwa wakijifunza na wakifunzwa stadi za lugha ya Kiswahili tangu darasa la kwanza. Wanafunzi walio katika madarasa ya chini hawakuchaguliwa kwani walichukuliwa kuwa na ujuzi wa chini katika stadi za lugha ya Kiswahili. Walimu wote wanaofunza somo la Kiswahili na hasa wanaofunza

wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika madarasa hayo manne katika shule hizo mbili jumuishi za msingi waliteuliwa pia. Walimu watano walilengwa katika shule jumuishi ya msingi ya Joel Omino na vilevile, katika shule jumuishi ya msingi ya Menengai walimu watano walilengwa pia.

Mtafiti alichagua asilimia kumi ya wanafunzi wote wasio na ulemavu wa macho katika darasa la nne, la tano, la sita na la saba. Katika shule jumuishi ya msingi ya Joel Omino wanafunzi ishirini na wawili katika darasa la nne, ishirini na sita katika darasa la tano, ishirini na watano katika darasa la sita na ishirini na wanne katika darasa la saba wasio na ulemavu wa macho waliteuliwa. Ilhali katika shule jumuishi ya msingi ya Menengai wanafunzi ishirini katika darasa la nne, kumi na tisa katika darasa la tano, ishirini katika darasa la sita na kumi na tisa katika darasa la saba wasio na ulemavu wa macho waliteuliwa pia.

1.8.4 Mbinu za Ukusanyaji Data

Utafiti huu ulihusisha mbinu tatu za kukusanya data; uchunzaji, hojaji na mahojiano. Nyanjani, mtafiti alitumia mbinu ya uchunzaji kuwatazama wanafunzi wa madarasa ya nne, tano, sita na ya saba. Mbinu ya uchunzaji ilitumika kuchunguza uhusiano wa mwalimu anapofunza na kuongoza kila shughuli darasani huku mwanafunzi akifuata maagizo na kujifunza. Aidha, mbinu ya uchunzaji ilitumika kuchunguza mazingira ya darasani na shuleni katika shule jumuishi ya msingi ya Menengai na Joel Omino ambapo ujifunzaji hufanyika. Mbinu ya mahojiano ilitumika kwa wanafunzi wote walio na ulemavu wa macho na kwa baadhi ya walimu wa Kiswahili kwa kupata data kuhusu ujifunzaji stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi walio na ulemavu wa

macho katika shule jumuishi katika Kaunti za Nakuru na Kisumu. Vilevile, hojaji ilitumika kwa wanafunzi wote walio na ulemavu wa macho na pia kwa baadhi ya wanafunzi wasio na ulemavu wa macho.

Wanafunzi wenye ulemavu wa macho walihojiwa katika vikundi vinne ambapo wanafunzi walio katika darasa moja waliwekwa katika kikundi kimoja ili wajengane kwa hoja. Mtafiti aliyarekodi yote yaliyo muhimu yaliyomwezesha kukamilisha utafiti lengwa kwa kupata data toshelevu. Njia ya mahojiano ilikuwa na umuhimu kwani si kila habari ilipatikana kwa njia ya uchunguzaji. Utafiti wa awali ulifanywa na mtafiti katika shule jumuishi ya Menengai na Joel Omino. Data iliyokusanywa ilirekodiwa kwa kutumia kinasa sauti na ilisaidia kujibu maswali ya utafiti.

1.8.5 Maadili ya Utafiti

Uchunguzi huu ulizingatia maadili mbalimbali. Kwanza kabisa, barua ya utambulisho iliombwa kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta. Pili, kibali kiliombwa kutoka kwa kamati ya kutathmini maadili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta (CRES) na kisha kwa tume ya kitaifa ya teknolojia ya sayansi na uvumbuzi (NACOSTI). Vilevile, kibali kiliombwa kutoka kwa kamishina na mkurugenzi wa Kaunti ya Nakuru na Kisumu na mwalimu mkuu wa shule jumuishi ya msingi ya Menengai na Joel Omino. Utafiti huu ulihakikisha kuwa data iliyokusanywa ni ile ambayo watafitiwa walikubali kuitoa kwa hiari yao. Aidha, majina ya lakabu yalitumika ili kuficha utambulisho wa watafitiwa. Watafitiwa watapata habari ya jinsi data ilihifadhiwa. Mtafiti atahakikisha kuwa watafitiwa watapata nakala ya ripoti ya utafiti huu ikiwa wataiomba.

1.8.6 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa ilichanganuliwa kwa kuzingatia maswali, malengo na nadharia ya utafiti na matokeo kuwasilishwa kwa njia iliyolinganisha ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule jumuishi katika Kaunti za Nakuru na Kisumu. Aidha, mihimili ya nadharia ya Usomi Tendaji iliongoza kuchanganua data iliyokusanywa kutokana na mahojiano, hojaji na uchunzaji.

1.8.7 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo ambapo dondoo ya waliyoyasema walimu na wanafunzi zilitolewa. Aidha, majedwali na chati yalitumika. Matokeo ya data yalizingatia ujifunzaji wa stadi za kiswahili kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule jumuishi ya Menengai na Joel Omino.

1.9 Hitimisho

Sura hii kwa jumla imezingatia utaratibu uliofuatwa ili kufanikisha utafiti huu. Utaratibu huu ni pamoja na usuli wa mada unaohusiana na ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya kinadharia na vilevile mbinu za utafiti zilizotumiwa. Sura inayofuata imeshughulikia tofauti za changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi za Menengai na Joel Omino katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili.

SURA YA PILI

TOFAUTI ZA CHANGAMOTO ZINAZOWAKUMBA WANAFUNZI WENYE ULEMAVU WA MACHO KATIKA SHULE JUMUISHI KATIKA UJIFUNZAJI WA LUGHA YA KISWAHILI

2.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia tofauti za changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi za msingi za Menengai na Joel Omino katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili. Sura hii iliongozwa na mihimili miwili ya nadharia ya Usomi Tendaji ya Bruner (1966); ili ufunzaji na ujifunzaji uwe bora, maandalizi yanafaa kufanywa kabla ya somo na watu hujifunza zaidi wakati wanajifunza na watu wengine kuliko wakati wanajifunza peke yao. Majina ya lakabu yalitumika ili kuficha utambulisho wa watafitiwa. Changamoto ambazo mtafiti alibaini kutokana na uchanganuzi wa data ni kama zifuatazo; muda wa ufunzaji na ujifunzaji, ukosefu wa ujuzi wa walimu, idadi kubwa ya wanafunzi madarasani, mtazamo hasi wa wanafunzi na walimu, ukosefu wa vitabu vifaavyo na vifaa vya ufunzaji na ujifunzaji, idadi ndogo ya walimu wanaofunza somo la Kiswahili, kutegemea wanafunzi wasio na ulemavu wa macho, ushirikiano kutoka kwa wazazi, hali ya umaskini na maeneo ambapo shule inapatikana. Mtafiti alizigawa changamoto hizi katika matapo matatu na kila changamoto ilishughulikiwa katika kila shule kivyake.

2.1 Changamoto Zinazotokana na Mazingira ya Darasani

Katika sehemu hii mtafiti amezungumzia changamoto zinazojitokeza katika muktadha wa darasa ambazo zinaathiri ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili katika shule jumuishi lengwa.

2.1.1 Muda wa Ufunzaji na Ujifunzaji

Katika mahojiano na walimu wa Kiswahili na wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule jumuishi za msingi za Joel Omino na Menengai, mtafiti alibaini kuwa muda wa kufunza na kufanya mitihani ulikuwa na changamoto kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Kwa mujibu wa walimu wote kumi waliohojiwa katika shule mbili lengwa, somo la Kiswahili lilifunzwa kwa dakika thelathini na tano peke yake, muda ambao haukutosha kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili hasa stadi ya kusoma na kuandika. Stadi hizi mbili zilionekana kuwa na changamoto kwa wanafunzi wenye ulemavu kulingana na hojaji walizozijaza.

Katika shule ya Menengai, mwalimu anayefunza darasa lililokuwa na mwanafunzi mwenye upofu kamili alisema kuwa stadi hizi mbili zilikuwa na changamoto kwani ilikuwa vigumu kumfuatilia mwanafunzi huyu ipasavyo huku akiwashughulikia wanafunzi wengine wasio na ulemavu wa macho ndani ya muda wa dakika thelathini na tano. Vilevile, kulingana na mwalimu huyu, ilibidi mwanafunzi asiye na ulemavu wa macho kumsaidia kwa kumsomea kitabu ili aweze kuandika kwa kutumia breli jambo ambalo huchukua muda mwingi. Isitoshe, kulingana naye, kazi ya mwanafunzi aliye na upofu kamili na walio na upungufu wa kuona hubidi kuangaliwa kwa umakini

zaidi na hili huchukua muda mrefu. Kinyume na mhimili wa nne wa nadharia ya Usomi Tendaji ya Bruner (1966) unaosisitiza kuwa, watu huweza kujifunza zaidi na watu wengine kuliko wanapojifunza peke yao ilibainika kuwa ni changamoto wanafunzi wenye ulemavu wa macho kujifunza pamoja na wanafunzi wasio na ulemavu wa macho katika darasa moja ndani ya muda uliotengewa somo la Kiswahili.

Mwalimu mwingine katika shule ya Menengai aliye na mafunzo ya kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho alidai kuwa baada ya kuwafunza somo la Kiswahili inabidi kuwapa baadhi ya wanafunzi darasani hasa walio na upofu kamili mafunzo maalum nje ya madarasa yao. Jambo hili huwa ni changamoto kwani muda haupatikani kutokana na masomo mengi ambayo wanafaa kushughulikia. Uchunzaji wa mtafiti ulibaini kuwa muda mwingi ulihitajika kusahihisha kazi ya ziada na mitihani ya wanafunzi walio na ulemavu wa macho. Hili lilitokana na kuwa kando na kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wasio na ulemavu wa macho katika darasa moja, ilimbidi msomaji wa breli ahusishwe katika kufasiri kazi iliyoandikwa na mwanafunzi mwenye upofu kamili ili mwalimu aisahihishe.

Hali hii pia ilijitokeza wazi katika shule ya Joel Omino. Mwalimu Neema, anayefunza darasa la sita na amefunza katika darasa hilo kwa miaka kumi alipohojiwa alikiri kuwa, hata baada ya kumweka mwanafunzi mwenye ulemavu wa macho karibu na ubao bado alichukua muda mwingi kuyasoma au kuyanakili maandishi yaliyo ubaoni kitabuni.

Mwalimu Neema pia alidai kuwa;

Kupitia uandishi wa insha ambapo wanafunzi huboresha stadi ya kuandika inadhihirika kuwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho huwa na maendeleo mabaya ya maneno na hati zisizo nadhifu ikilinganishwa na wanafunzi wasio na ulemavu wa macho. Hali hii hutokana na utaratibu wa mtalaa wa kufunza kwa muda wa dakika thelathini na tano ambao kwa kiasi fulani husababisha wanafunzi wenye ulemavu wa macho kuandika kwa kasi ili waweze kuwa katika kiwango sawa na wanafunzi wenzao wasio na ulemavu wa macho. Muda huu wa kufunza somo hili haumruhusu mwalimu kufuatilia jinsi kila mwanafunzi anaandika daftarinini mwake.

Maoni yaliyotolewa katika shule hizi mbili yanashabihiana na ya Haugann (1987) ambaye pia anasema kuwa wanafunzi walio na upungufu wa uwezo wa kuona wana uwezo wa kusoma maandishi ya kawaida, hata hivyo, wanachukua muda mwingi kusoma maandishi hayo ikilinganishwa na wanafunzi wasio na ulemavu wa macho. Anaendelea kusema kuwa, muda wanaochukua wakati wa kusoma ni mwingi kwani wanatatizika kuona maneno.

Walimu wa shule jumuishi ya msingi ya Menengai waliafikiana na wenzao katika shule ya Joel Omino. Isitoshe, walimu wote katika shule lengwa waliafikiana miongoni mwao kuwa muda wa ufunzaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili haukutosha kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Matokeo haya yanathibitisha kuwa, maandalizi mwafaka hayajafanywa ili muda wa ufunzaji na ujifunzaji uweze kuwatosha wanafunzi hawa na hivyo, yanaenda kinyume na mhimili wa pili wa nadharia ya Usomi Tendaji ya Bruner (1966) unaosisitiza kuwa, maandalizi yanafaa kufanywa kabla ya somo ili mwanafunzi aweze kushirikishwa katika kila hatua ya ujifunzaji na ndiposa changamoto hii ikajitokeza. Vifaa vya ufunzaji na mafunzo ya

kutosha yanapaswa kutolewa kwa walimu wa Kiswahili ili waweze kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu wa macho kumudu muda waliopewa kushughulikia ujifunzaji wao.

2.1.2 Ukosefu wa Ujuzi wa Walimu

Walimu wanne kati ya watano wanaofunza Kiswahili katika madarasa ya nne hadi ya saba katika shule jumuishi ya msingi ya Menengai walipohojiwa walisema kuwa hawana ujuzi wa kuwahudumia wanafunzi walio na ulemavu wa macho. Hata hivyo, mwalimu mmoja anayefunza darasa la saba alisema kuwa alihudhuria mafunzo akiwa kazini. Katika mahojiano, mtafiti alibaini kuwa mwalimu anayefunza darasa la tano lililokuwa na mwanafunzi aliye na upofu kamili hakuelewa jinsi ya kutumia breli wala kufasiri maneno yaliyoandikwa kwa breli. Mwalimu huyo alieleza kuwa ilimbidi kumhusisha msomaji wa breli ili aweze kumsaidia kufasiri kazi iliyoandikwa na mwanafunzi huyu ili aweze kuisahihisha. Kazi iliyofasiriwa kulingana na mwalimu huyu mara nyingi ilikuwa na makosa kwani msomaji wa breli anaweza kufasiri neno kinyume na maana ambayo mwanafunzi alikuwa amekusudia. Maoni haya yanaoana na maoni ya Mwakyeja (2013) anayesema kuwa hata kama walimu wanaelewa umuhimu wa ujumuishaji, wengi wao hawana ujuzi wa kusoma na kufasiri breli na vilevile, kuboresha mbinu za ujifunzaji wa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi.

Changamoto hii ilionekana pia katika shule jumuishi ya msingi ya Joel Omino ambapo walimu wanne kati ya watano wanaofunza somo la Kiswahili walisema kuwa hawajatayarishwa kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika

madarasa ya kawaida. Jambo hili lilileta ugumu katika kuwapa umakini ufaao. Aidha, kwa mujibu wa walimu hawa, warsha hazikutayarishwa kuwapa mafunzo wakiwa kazini. Matokeo haya yanaakisi maoni ya Otyola na wenzake (2017) wanaoshikilia kuwa walimu wengi wanaofunza wanafunzi wenye ulemavu wa macho hawajapewa mafunzo ya kuwashughulikia wanafunzi hawa katika madarasa jumishi. Maoni ya Otyola na wenzake (2017) yanaungwa mkono na Basaran (2012) ambaye anasema kuwa, programu za mafunzo ya walimu wa lugha wanaofunza katika shule za wanafunzi wenye ulemavu wa macho wakiwa kazini, zinapaswa kutathminiwa upya na kufanywa kuwa bora zaidi. Vilevile, kozi kuhusu ufunzaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum inapaswa kujumuishwa. Kozi hizo kulingana naye zinafaa kuzingatia sifa za wanafunzi wenye ulemavu wa macho kama vile matumizi yao ya maneno na pia kuisitiza umuhimu wa teknolojia za kidijitali katika kukuza stadi za lugha za kusikiliza na kuzungumza.

2.1.3 Idadi Kubwa ya Wanafunzi Madarasani

Uchunzaji uliofanywa na mtafiti ulionyesha kwamba kulikuwa na idadi kubwa ya wanafunzi madarasani katika shule jumishi za msingi za Menengai na Joel Omino. Jedwali 2.1 linaorodhesha idadi ya wanafunzi katika shule za Menengai na Joel Omino kama ifuatavyo:

Jedwali 2.1: Idadi ya Wanafunzi katika Shule Jumuishi za Menengai na Joel Omino

Darasa	Idadi ya Wanafunzi			
	Shule ya Menengai		Shule ya Joel Omino	
	Walio na Ulemavu wa Macho	Wasio na Ulemavu wa Macho	Walio na Ulemavu wa Macho	Wasio na Ulemavu wa Macho
4	3	210	1	255
5	3	195	2	267
6	1	204	3	258
7	2	216	2	261
Jumla	9	825	8	1041

Walimu waliohojiwa katika shule ya Menengai walisema kuwa kila darasa lilikuwa na wanafunzi takriban sabini. Madarasa haya yalikuwa na changamoto kubwa hasa wakati wa kuwasilisha somo la Kiswahili darasani na vilevile, kusahihisha vitabu vya wanafunzi kama alivyoeleza mwalimu Amina;

Kuna uwezekano wa wanafunzi wenye ulemavu wa macho kusahaulika kabisa kwa kuwa idadi yao ni ndogo miongoni mwa wanafunzi wengi wasio na ulemavu wa macho, kwa mfano katika darasa ambalo lina wanafunzi wawili wenye ulemavu wa macho miongoni mwa wanafunzi sabini na wanne kuna uwezekano mkubwa wa wanafunzi wasio na ulemavu wa macho kupewa umakini zaidi kwani ni wengi.

Haya yaliungwa mkono na mwalimu Zawadi aliyedai kuwa;

Mwalimu anapofunza stadi za lugha ya Kiswahili katika darasa lenye idadi kubwa ya wanafunzi yeye huwa na majukumu mazito ya kutekeleza hivi kwamba, mwanafunzi aliye na ulemavu wa macho hafuatiliwi kwa namna ipasavyo.

Kama inavyodhihirika katika jedwali 2.1, hali ilikuwa vivyo hivyo katika shule ya Joel Omino ambapo madarasa yalikuwa na idadi kubwa ya wanafunzi kupita kiasi.

Mahojiano na uchunguzi uliofanywa na mtafiti ulionyesha kuwa kila darasa lilikuwa na wanafunzi takriban tisini. Walimu waliohojiwa walisema kuwa madarasa hayo makubwa yalikuwa na athari hasi kwa wanafunzi wote na hasa kwa wale wenye ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kama alivyoeleza mwalimu Ali;

Wakati wa ujifunzaji wa stadi za lugha kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho, idadi kubwa ya wanafunzi darasani huwa kuzuizi. Kwa mfano, wakati wa kujifunza stadi ya kusoma kupitia usomaji wa hadithi, wakati mwingine inafaa mwalimu atumie modeli maalum ili kuelezea dhana fulani kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho lakini hili halifanyiki mara nyingi kwani ni vigumu kumshughulikia mwanafunzi mmoja au wawili katika muda mchache.

Uchunguzi katika shule hii ulionyesha kuwa walimu walitoa mafunzo yao kwa kutumia mbinu ya mhadhara ili kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho na walipohojiwa kuhusu mbinu hii walisema kuwa kuandika ubaoni kulichukua muda mwingi ambao hawakuwa nao. Hali hii inakinzana na maoni ya Otyola na wenzake (2017) wanaoeleza kuwa mbinu ambayo walimu wanatumia kufunzia ambayo ni mbinu ya mhadhara na kuamuru kwa maelezo hairuhusu ufunzaji na ujifunzaji sahihi kwa wanafunzi.

Matokeo haya yanadhihirisha wazi kuwa kuna uwezekano wa wanafunzi wenye ulemavu wa macho kusahaulika kabisa kutokana na idadi yao ndogo miongoni mwa wanafunzi wengi wasio na ulemavu wa macho darasani. Hii inaenda kinyume na mhimili wa pili wa nadharia ya Usomi Tendaji ya Bruner (1966) unaoshikilia kuwa,

mwanafunzi anafaa kushirikishwa kwa kiasi kikubwa katika kila mchakato tendi wa ujifunzaji ili kuibua dhana mpya na si mwalimu kumwekea dhana akilini.

2.1.4 Mtazamo Hasi wa Walimu na Wanafunzi

Changamoto nyingine iliyojitokeza bayana ni mtazamo hasi wa walimu na wanafunzi katika ufunzaji na ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika. Walimu wanne kati ya watano wanaofunza Kiswahili katika shule ya Menengai walieleza kuwa, walikuwa na mtazamo hasi kuhusu ujumuishaji kwani kulingana nao unawapotezea wakati wa kuwashughulikia wanafunzi wasio na ulemavu wa macho. Mwalimu mmoja tu ndiye alikuwa na mtazamo chanya kuhusu ujumuishaji wa wanafunzi. Mtazamo huu chanya ulitokana na kuwa mwalimu huyu alikuwa amepata mafunzo maalum ya kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Mtafiti alipohudhuria somo la Kiswahili katika darasa la tano lililokuwa na mwanafunzi mmoja aliyekuwa na upofu kamili na mwingine upungufu wa kuona katika shule ya Menengai, alishuhudia mwalimu akifunza wanafunzi wote stadi ya kusoma na kuandika sawia bila kuwapa wanafunzi hao umakini ufaao.

Katika shule ya Joel Omino mtazamo hasi pia ulidhihirika kutokana na hojaji za wanafunzi wasio na ulemavu wa macho. Baadhi yao walisema kuwa kushirikiana na wanafunzi wenye ulemavu wa macho hasa katika ujifunzaji wa stadi za kuandika na kusoma kulikuwa si jambo walilofanya kwa hiari yao bali ni kwa kulazimishwa na mwalimu. Mwalimu anayefunza Kiswahili katika darasa la tano aliye na ujuzi wa kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho alithibitisha haya kwa kutueleza kuwa, asilimia kubwa ya walimu wapya wanaojiunga na shule hiyo ambao hawana

ujuzi wa kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho huwa na mtazamo hasi na kuwa kubadilisha mtazamo huo huchukua muda. Hili huwa na athari hasi kwa ujifunzaji wa wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Maoni haya yanalingana na ya Jobe na wenzake (1996) ambao wanasema kuwa kuna tofauti kubwa katika mtazamo baina ya walimu walio na mafunzo ya kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu katika madarasa jumuishi ikilinganishwa na wasio na mafunzo. Kulingana na Jobe na wenzake (1996), wale walio na mafunzo wana mtazamo chanya wa kuwahudumia wanafunzi wenye ulemavu wa macho na hawawabagui ikilinganishwa na wasio na mafunzo. Walimu kuwa na mtazamo chanya kuhusu elimu jumuishi, kulingana na Kuyini na Desai (2007) huwasaidia walimu kukuza mbinu za kufundishia ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho.

2.1.5 Ukosefu wa Vitabu Vifaavyo na Vifaa vya Ufunzaji na Ujifunzaji

Lengo kuu la kutumia vifaa vya ujifunzaji ni kuboresha mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji (Marfo na wenzake, 2020). Uchunzaji na mahojiano na walimu kutoka shule mbili lengwa zilionyesha kuwa vitabu vilivyochapishwa kwa breli na vilivyo katika maandishi makubwa havikuwepo. Aidha, walimu wote walikubaliana kuwepo kwa ukosefu wa vifaa vya ufunzaji na ujifunzaji. Walimu hawa walikiri kuwa, serikali mara nyingi haitoi vifaa vinavyoboresha ujifunzaji na iwapo itatoa, vifaa hivyo huchelewa. Hili likifanyika, husababisha wanafunzi kubaki nyuma na hasa wanafunzi wenye ulemavu wa macho wanaohitaji vifaa vyao maalum vinavyowasaidia kuwa katika kiwango kimoja na wenzao wasio na ulemavu wa macho. Mfano wa vifaa vya ujifunzaji vya wanafunzi wenye ulemavu wa macho kulingana na walimu waliohojiwa na mtafiti ni kama vile, matumizi ya vipakatalishi vilivyo na sauti, redio na rununu zenye sauti,

matumizi ya modeli na vifaa halisi na matumizi ya chati zenye rangi tofauti tofauti kwa wanafunzi walio na upungufu wa kuona. Hata hivyo, kulingana na walimu hawa ni changamoto kubwa kuvipata vifaa hivi.

Walimu waliohojiwa katika shule ya Menengai walisema kuwa vitabu vilivyochapishwa kwa breli vilikuwepo, hata hivyo, vilikuwa vya mtalaa wa kitambo uliokuwa umepitwa na wakati. Kuhusu vitabu vilivyo katika maandishi makubwa mwalimu Juma alisema kuwa;

Vitabu vya Kiswahili vilivyo katika maandishi makubwa havipo kabisa kwani gharama ya kuvichapisha huwa juu sana. Kwa mfano, ili kuchapisha ukurasa mmoja wa kitabu hiki itamgharimu anayechapisha shilingi kumi na saba. Hivyo basi, kuchapisha kitabu kizima kutakuwa na changamoto kubwa. Ukosefu wa vitabu hivi huathiri uboreshaji wa stadi ya kusoma kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho kwani hutatizika kusoma vitabu vya kawaida na hivyo basi, kuchukua muda mwingi kujifunza ikilinganishwa na wenzao wasio na ulemavu wa macho.

Katika shule ya Joel Omino hali ilikuwa vivyo hivyo, kwani wanafunzi wenye ulemavu wa macho na walimu waliafikiana na yale walimu katika shule ya Menengai waliyasema. Mwalimu Ali alidai kuwa;

Vitabu vya Kiswahili vilivyo katika maandishi makubwa havipo kabisa ilhali vifaa vya ufunzaji na ujifunzaji ni changamoto kubwa shuleni humu kwani havipatikani na vile ambavyo vinapatikana ni vichache mno hivi kwamba wanafunzi wenye ulemavu wa macho hupata matatizo kufuatilia somo la Kiswahili. Kwa mfano, wanafunzi ambao wana upungufu wa kuona hutumia bodi nyeupe lakini bodi hizi haziwatoshi wanafunzi hawa. Aidha, walimu hawapendi kutumia bodi hizi kwani wanadai kuwa muda hautoshi wa kuandikia wanafunzi wasio na ulemavu wa macho ubaoni na kwa upande mwingine kuwaandikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika bodi hizi nyeupe katika somo moja.

Maoni ya walimu na wanafunzi katika shule hizi mbili yanalingana na ya Simon na wenzake (2010) na Sikanku (2018) wanaosema kuwa changamoto kubwa inayowakabili wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi ni ukosefu wa vitabu vilivyochapishwa kwa breli na vifaa vya ujifunzaji vya kutosha vinavyowasaidia katika mchakato wa ujifunzaji katika shule jumuishi. Haugann (1987) anashadidia kuwa, wanafunzi wenye ulemavu wa macho hukabiliwa na changamoto kubwa ya kuvipata vitabu vya kusoma katika breli, katika maandishi makubwa na katika kanda.

Maoni ya Adetoro (2012) yanakinzana na ya Haugann (1987) anayedai kuwa kuna ongezeko kubwa la matumizi ya vitabu vilivyo na sauti ikilinganishwa na matumizi ya vitabu vilivyochapishwa kwa breli na vitabu vilivyo katika maandishi makubwa miongoni mwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Kutokana na wataalam Simon na wenzake (2010), Sikanku (2018), Haugann (1987) na Adetoro (2012) tunaweza kusema kuwa ili ufunzaji na ujifunzaji kamili wa stadi za lugha katika shule jumuishi ufikiwe lazima kuwepo kwa vifaa na vitabu vya wanafunzi wenye ulemavu wa macho na hili litafanikisha mazingira mazuri kwa wanafunzi wote mtawalia. Kinyume na mhimili wa pili wa nadharia ya Usomi Tendaji ya Bruner (1966) unaoshikilia kuwa mwalimu anafaa kufanya maandalizi kabla ya somo ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata hamu ya kujifunza kwa kutumia vifaa kama vile picha, michoro, rekodi za sauti, modeli na vilevile, vitabu, matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwepo kwa changamoto ya ukosefu wa vitabu vifaavyo na vifaa vya ufunzaji na ujifunzaji. Ukosefu wa vifaa, gharama yake na matumizi ya nyenzo zilizopitwa na wakati hudumaza juhudi za

walimu za kufanya maandalizi ya awali ambayo yangewafaa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi.

2.1.6 Idadi Ndogo ya Walimu Wanaofunza Somo la Kiswahili

Shule zote mbili za Joel Omino na Menengai zilikuwa na idadi ndogo ya walimu wa somo la Kiswahili ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi wanaopatikana katika madarasa husika. Jedwali 2.2 linadhihirisha idadi ya walimu na wanafunzi katika madarasa mbalimbali ya shule za Joel Omino na Menengai.

Jedwali 2.2: Idadi ya Walimu na Wanafunzi katika kila darasa la Shule ya Joel Omino na Menengai

Darasa	Shule ya Menengai			Shule ya Joel Omino		
	Idadi ya Mikondo	Idadi ya Walimu	Idadi ya Wanafunzi	Idadi ya Mikondo	Idadi ya Walimu	Idadi ya Wanafunzi
4	3	1	213	3	2	256
5	3	1	198	3	2	269
6	3	2	205	3	1	261
7	3	2	218	3	2	263
Jumla	12	6	834	12	7	1049

Kutokana na Jedwali 2.2, shule ya Joel Omino ilikuwa na walimu saba wanaofunza somo la Kiswahili katika madarasa kumi na mawili kutoka darasa la nne mpaka la saba na kila moja lilikuwa na wanafunzi takriban tisini. Vilevile, hali hii ilidhihirika katika shule jumuishi ya Menengai ambayo ilikuwa na walimu sita katika madarasa kumi na mawili; kila darasa likiwa na wanafunzi takriban sabini. Kutokana na takwimu ya wanafunzi na walimu katika shule hizi, ni wazi kuwa idadi ya walimu ni chache ikilinganishwa na wanafunzi wanaopatikana katika darasa moja.

Data kutokana na uchunguzi zinaonyesha kuwa idadi kubwa ya wanafunzi ilikuwa changamoto kwa walimu wanapofunza na hivyo basi, wanafunzi walio na ulemavu wa macho hawapewi wakati maalum hasa somo linapohitaji maelezo ya kina kama vile uandishi wa insha na kusoma darasani. Wakati mwingine, walimu hutoka darasani bila kutangamana na wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa stadi za lugha. Idadi ya wanafunzi kwa walimu katika shule hizi jumuishi inakinzana na maoni ya Cook na wenzake (2017) ambao wanasema kuwa ili kufanikiwa katika kukuza tabia na mtagusano mzuri kati ya wanafunzi na walimu lazima kuwepo na uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi watano.

Matokeo ya utafiti katika shule lengwa yanadhihirisha kuwa idadi ya walimu ni chache ikilinganishwa na wanafunzi wanaopatikana katika darasa moja. Hii ni changamoto kwani inaenda kinyume na mhimili wa nne wa nadharia ya Usomi Tendaji unaosisitiza kuwa, watu huweza kujifunza zaidi wakati wanajifunza na watu wengine kuliko wakati wanajifunza peke yao. Kungalikuwa na idadi ifaayo ya uwiano wa mwalimu kwa wanafunzi usomi tendaji ungedhihirika vizuri katika madarasa ambayo wanafunzi wenye ulemavu wa macho wanapatikana na labda changamoto hii haingekuwepo.

2.1.7 Kutegemea Wanafunzi Wasio na Ulemavu wa Macho

Wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule hizo mbili jumuishi waliwategemea wanafunzi wenzao wasio na ulemavu wa macho kwa kiasi kikubwa katika ujifunzaji wa stadi za lugha. Hii ilikuwa moja kati ya changamoto nyingi zilizojitokeza. Hali hii ilidhihirika kupitia mbinu ya uchunguzi katika shule ya Menengai ambapo mwanafunzi mwenye upofu kamili aliwategemea wenzake wasio na ulemavu wa macho katika

ujifunzaji. Baada ya mwalimu kutoa mhadhara, aliwapa wanafunzi kazi ya ziada ambapo ilimbidi mwanafunzi mmoja amsomee mwanafunzi huyo maswali huku akiendelea kuandika kazi yake. Kumtegemea mwanafunzi huyu asiye na ulemavu wa macho kuliwafanya wanafunzi hawa wawili kuchukua muda mwingi ili kukamilisha kazi.

Isitoshe, ilibainika kutokana na mahojiano ya walimu kuwa mwanafunzi mwenye ulemavu wa macho hakuwa na maendelezo mazuri ya maneno kwa kuwa kuna uwezekano wa mwanafunzi anayemsomea maswali kuacha maneno fulani kutokana na kufanya kazi nyingi kwa wakati mmoja. Aidha, wanafunzi walio na upungufu wa kuona waliosailiwa katika shule hii walisema kuwa hawakuona vielelezo vilivyo ubaoni vizuri na hivyo basi, iliwabidi kuwapa muda wanafunzi wenzao wasio na ulemavu wa macho wanakili kilicho ubaoni vitabuni mwao ili wayapakue kutoka vitabu hivyo vyao.

Changamoto hii ilidhihirika sawia katika shule ya Joel Omino ambapo wanafunzi waliohojiwa walisema kuwa matatizo ya kuona ubaoni yaliwafanya wawategemea wanafunzi wenzao wasio na ulemavu wa macho ili waweze kufuata maagizo na mafunzo yanayotolewa na mwalimu. Walimu pia walitoa kauli zinazowiana na zile zilizotolewa na wanafunzi kwani kulingana nao ilikuwa rahisi kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho kuachwa nyuma kielimu na wenzao wasio na ulemavu wa macho katika madarasa jumuishi kutokana na hali ya kutegemeana. Matokeo haya yanaakisi maoni ya Kapur (2018) anayesema kuwa kwa kawaida wanafunzi wenye ulemavu wa macho huwategemea wenzao katika ujifunzaji wao. Anaendelea kusema kuwa shuleni,

wanafunzi hawa huwategemea walimu na wanafunzi wenzao ilhali nyumbani wanawategemea wazazi na jamaa zao.

Ni wazi kuwa, wanafunzi wenye ulemavu wa macho wanawategemea wanafunzi wasio na ulemavu wa macho kwa kiasi kikubwa katika madarasa jumuishi. Kutokana na hali hii, wanafunzi walio na ulemavu wa macho hupata msaada kutoka kwa wenzao wasio na ulemavu wa macho. Haya ndiyo yanayoelekezwa na mhimili wa nne wa nadharia ya Usomi Tendaji ya Bruner (1966) unaosisitiza kuwa, mchakato wa ujifunzaji huwa bora zaidi wanafunzi wakijumuishwa kwani wao hujenga maana pamoja na hivyo basi, kuimarishana kiujuzi.

2.2 Changamoto Zinazotokana na Mazingira ya Nyumbani

Changamoto zinazojitokeza katika sehemu hii ni zile ambazo chanzo chake ni maeneo ya nyumbani, yaani mahali ambapo mwanafunzi mwenye ulemavu wa macho anatoka.

2.2.1 Ushirikiano Kutoka kwa Wazazi

Mtafiti alipowasaili walimu wa shule jumuishi ya msingi ya Joel Omino kuhusu changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho, mwalimu Nuru alidai kwamba;

Wazazi wengi hawana elimu kuhusu ulemavu wa macho hasa kule vijijini ambapo baadhi ya watoto wenye ulemavu wa macho wanatengwa kwa kutopelekwa shuleni. Aidha, baadhi yao wana imani za kishirikina kuhusu ulemavu. Isitoshe, hata baada ya wanafunzi wengine kupimwa shuleni na kupatikana kuwa wana ulemavu wa macho, wazazi wengine hupinga kuwa watoto wao hawana matatizo yoyote na hivyo basi, hawawashughulikii kama wanafunzi wanaohitaji msaada wa ziada bali kama wanafunzi wasio na ulemavu wa macho. Wengi wao hawanunui vifaa vinavyohitajika kama vile miwani kwani hawaamini kuwa watoto wao wana shida.

Matokeo yaliyodhihirika katika shule ya Joel Omino yanaoana na maoni ya Maemba na wenzake (2016) wanaodai kuwa kuna baadhi ya wazazi ambao wana dhana mbaya kuhusu ulemavu wa macho. Kulingana nao dhana hii wakati mwingine hutokana na baadhi ya wazazi kuona ulemavu wa macho kama laana.

Hata hivyo, hali hii haikudhihirika wazi katika shule ya Menengai kwani mwalimu mmoja kati ya watano waliosailiwa alisema kuwa wazazi ambao wana watoto wenye ulemavu wa macho katika shule hii walishirikiana na walimu wa somo la Kiswahili katika kuwashughulikia wanafunzi hawa. Aliendelea kudai kuwa wazazi ambao wana watoto wenye ulemavu wa macho katika shule hii walipewa mafunzo ya jinsi ya kuwashughulikia. Jambo ambalo walimu wengine walikubaliana nalo kutokana na mahojiano yaliyotekelezwa na mtafiti. Mwalimu huyu alipeana mfano kwa kusema kuwa;

Katika ujifunzaji wa stadi hasa stadi ya kusoma ambayo huwa na changamoto kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho, wazazi huwasaidia kuboresha stadi hii sanasana wanapofanya kazi ya ziada nyumbani. Kwa mfano, mwanafunzi aliye na upofu kamili huwa habebi mashine ya breli anapoenda nyumbani kutokana na uhaba wa mashine hizi. Anapopewa kazi ya ziada iliyofasiriwa na msomaji wa breli, mzazi wake humsomea maswali na kisha mwanafunzi huyu anapojibu, mzazi wake huandika chini majibu na kisha mwanafunzi humpelekea mwalimu shuleni kusahihisha.

Kutokana na utafiti uliotekelzwa ni dhahiri kuwa kuna tofauti ya kimtazamo kati ya mazingira ya mjini na mazingira ya kijijini. Wakazi wa mjini wana uelewa mzuri zaidi

kuhusu ulemavu kuliko watu wasio wa mjini ambao mtazamo wao kuhusu ulemavu ni finyu.

2.2.2 Hali ya Umaskini

Mojawapo ya changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho ni hali ya umaskini. Uchunzaji katika shule mbili lengwa ulionyesha kuwa baadhi ya wanafunzi hawakuwa na miwani na vifaa vingine vinavyoimarisha kiwango chao cha kuona kama vile darubini. Hali hii ilidhihirika wazi hasa kutokana na wanafunzi wenye ulemavu wa macho kuonyesha hali ya kutatizika wakati wa kusoma na kuchukua wakati mwingi wakati wa kuandika madaftarini. Hoja hii inaingiliana na mahojiano yaliyofanywa na mtafiti kwa walimu wa shule zote mbili ambao pia walishadidia kuwa baadhi ya wanafunzi ambao walikuwa wanawafunza hawakuwa na ala za macho kama vile miwani na darubini zinazohitajika katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili. Mathalan, katika shule ya Menengai wanafunzi watatu hawakuwa na ala za macho na walipohojiwa walisema kuwa hili lilitokana na wazazi wao kutoweza kumudu kununua ala hizi.

Vilevile, wanafunzi waliohojiwa katika shule ya Joel Omino walikiri kuwa wazazi wao hawangeweza kununua vifaa vya ujifunzaji. Mtafiti alipowahoji wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika majopo, mwanafunzi mmoja katika shule ya Joel Omino alidokeza kuwa;

Mimi hupata changamoto ninapojifunza somo la Kiswahili kwani ili kuona kile ambacho mwalimu ameandika ubaoni na kile ambacho kipo kitabuni hunibidi nishirikiane na wenzangu wasio na ulemavu wa macho ili niweze kuyapata maelezo kwa ufasaha kwani sina ala za macho kama vile miwani. Hii ni kutokana na mzazi wangu kutokuwa na uwezo wa kuninunulia ala hizi. Isitoshe, hata kununua vitabu vya kusoma ni changamoto kubwa. Hili huniathiri wakati wa kufanya kazi ya ziada.

Mwanafunzi wa pili alichangia maoni ya mwanafunzi wa kwanza kwa kuendeleza kuwa;

... hata mimi sina miwani kwani mzazi wangu hana uwezo wa kuninunulia na hili huleta matatizo hasa ninaposoma kitabuni na ubaoni. Vilevile, ninapofanya mitihani ninatatizika na hasa wakati wa uandishi wa insha.

Aidha, ilibainika kuwa, wanafunzi mia moja na wawili kati ya wanafunzi mia moja na watano walioteuliwa walitoka katika vitongoji duni vya Nyalenda kulingana na hojaji walizozijaza. Vitongoji ambavyo wakazi wake wana sifa ya kuwa na kipato cha chini na hivyo basi, hali ya umaskini ni ya kiwango cha juu. Shrestha (2017) anaeleza kuwa hali ya umaskini huwaathiri baadhi ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho na hili huunda vizuizi katika elimu yao, uchunguzi wa mara kwa mara hospitalini na kwa kushiriki katika shughuli zingine za kujiendeleza. Anaendelea kudokeza kuwa matumizi ya ala za macho ambazo ni ghali na vilevile, vifaa vya kusoma vilivyo vya bei ya juu huwa changamoto kubwa wakati wa ujifunzaji kwani wengi wao hawawezi kumudu vifaa hivi. Maoni yake Shrestha (2017) yanalingana na ya Hannum na Zhang (2012) wanaosema kuwa wanafunzi wasio na uwezo wa kuona kile mwalimu ameandika ubaoni na kufanya kazi ya ziada hukabiliwa na vizuizi dhahiri vya ujifunzaji.

2.3 Changamoto Zinazotokana na Mazingira ya Shuleni

Katika sehemu hii mtafiti amezungumzia changamoto inayoathiri ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili inayojitokeza kutokana na shule jumuishi kupatikana katika eneo fulani kijiografia.

2.3.1 Maeneo ambapo Shule Inapatikana

Uchunguzi uliotekeleza nyanjani ulibaini kuwa shule jumuishi ya msingi ya Menengai inapatikana katika mazingira ya mjini. Mazingira ambayo mtafiti alibaini kuwa na kelele wakati wa ujifunzaji. Mwalimu Amina aliyehojiwa alisema kuwa;

Kuna kelele humu shuleni kutokana na shule hii kuwa katikati ya barabara mbili kuu ambapo magari hupita. Aidha, wakati mwingine treni pia hupita. Kelele hii huwa na athari hasi wakati wa ufunzaji na ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwani wanafunzi wenye ulemavu wa macho hutegemea stadi ya lugha ya kusikiliza kwa kiasi kikubwa ili kupata mafunzo.

Tofauti na shule ya Menengai, changamoto ya kelele za kutoka barabarani haikudhihirika katika shule ya Joel Omino kwani shule hii inapatikana nje ya mji wa Kisumu. Kulingana na Lewis na wenzake (2017), uhusiano bora kati ya walimu na wanafunzi hutegemea vipengele kama vile kiwango cha kelele, hewa safi na mwangaza uliopo. Wanaendelea kusema kuwa, ikiwa vipengele hivyo havitazingatiwa vizuri huwa na athari hasi kwa mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji hasa kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho kwa kuwa ujifunzaji wao hutegemea zaidi stadi ya kusikiliza. Jedwali 2.3 linadhihirisha ulinganishaji wa changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi lengwa kama ifuatavyo:

Jedwali 2.3: Ulinganishaji wa Changamoto Zinazowakumba Wanafunzi wenye Ulemavu wa Macho katika Shule Lengwa

Changamoto	Menengai	Joel Omino
Muda wa Ufunzaji na Ujifunzaji	✓	✓
Ukosefu wa Ujuzi wa Walimu	✓	✓
Idadi Kubwa ya Wanafunzi Madarasani	✓	✓
Mtazamo Hasi wa Walimu na Wanafunzi	✓	✓
ukosefu wa vitabu vifaavyo na vifaa vya ufunzaji na ujifunzaji	✓	✓
Idadi Ndogo ya Walimu Wanaofunza Somo la Kiswahili	✓	✓
Kutegemea Wanafunzi Wasio na Ulemavu wa Macho	✓	✓
Ushirikiano Kutoka kwa Wazazi	×	✓
Hali ya Umaskini	✓	✓
Maeneo ambapo shule inapatikana	✓	×

Jedwali 2.3 linaonyesha changamoto zilizopatikana kutokana na uchunguzi uliotekelezwa katika shule mbili jumuishi. Alama (✓) inaonyesha kuwepo kwa changamoto hiyo ilhali alama (×) inaonyesha kutokuwepo kwa changamoto hiyo katika shule iliyotajwa. Changamoto nyingi zinawiana katika shule lengwa. Hata hivyo, kuna tofauti katika hoja ya ushirikiano kutoka kwa wazazi na vilevile, maeneo ambapo shule inapatikana. Tofauti hizi zitashughulikiwa katika sura inayofuata.

2.4 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia tofauti za changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho yaani wenye upungufu wa kuona na wenye upofu kamili. Mtafiti amezigawa changamoto hizo katika matapo matatu yaani; changamoto zinazotokana na mazingira ya darasani, nyumbani na shuleni. Maarifa katika sura hii, yalitusaidia kuelewa kwa uwazi tofauti za usuli wa mazingira na athari za tofauti hizo katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili. Masuala haya yalitusaidia kujenga sura zinazofuata.

SURA YA TATU

TOFAUTI ZA USULI WA MAZINGIRA YA UJIFUNZAJI KATI YA SHULE

JUMUISHI YA MENENGAI NA JOEL OMINO

3.0 Utangulizi

Sura ya pili ilishughulikia tofauti za changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi za msingi za Menengai na Joel Omino katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili. Sura hii, imeshughulikia tofauti za usuli wa mazingira ya ujifunzaji kati ya shule jumuishi ya Menengai na Joel Omino. Tofauti hizi ni kama vile; tofauti ya walimu wa kiswahili kati ya shule mbili lengwa, tofauti ya ushirikiano wa wazazi kati ya shule ya menengai na joel omino, tofauti ya tajiriba ya walimu kati ya shule jumuishi lengwa, tofauti ya upatikanaji wa chumba maalum katika shule lengwa na tofauti ya usuli wa lugha kati ya shule ya menengai na joel omino. Hapa mtafiti amelinganisha usuli wa mazingira kati ya shule jumuishi ya Menengai inayopatikana mjini ambapo kwa kawaida, kuna wingi lugha na shule jumuishi ya Joel Omino ambayo asilimia kubwa ya wanafunzi katika shule hii inazungumza lugha moja ya kwanza. Sura hii inaongozwa na mihimili miwili ya nadharia ya Usomi Tendaji ya Bruner (1966); kujifunza lazima kuanze na masuala ambayo yanapatikana katika mazingira ya wanafunzi ambayo wanajaribu kikamilifu kuunda maana na watu huweza kujifunza zaidi wakati wanajifunza na watu wengine kuliko wakati wanajifunza peke yao.

3.1 Tofauti ya Walimu wa Kiswahili kati ya Shule Mbili Lengwa

Mojawapo ya tofauti ya kimazingira mtafiti alitambua katika shule lengwa ni kuwepo kwa mwalimu mwenye ulemavu wa macho anayefunza somo la Kiswahili. Kutokana na uchunzaji, utafiti huu ulibaini kuwa shule ya Menengai ilikuwa na mwalimu mmoja mwenye ulemavu wa macho, yaani upofu kamili. Ilidhihirika kuwa wanafunzi katika madarasa ambayo mwalimu huyu anafunza walikuwa na uhusiano mzuri na yeye alipokuwa akitoa maagizo na kuongoza kila shughuli darasani hasa kupitia stadi ya kuzungumza na kusikiliza.

Aidha, kupitia mahojiano na wanafunzi waliokuwa na ulemavu wa macho, utafiti ulibaini wanafunzi hawa walijitambulisha na mwalimu huyu katika mchakato wa ujifunzaji wa stadi za lugha katika somo la Kiswahili. Matokeo haya yanathibitisha kuwa, watu huweza kujifunza zaidi wakati wanajifunza na watu wengine kuliko wakati wanajifunza peke yao, hali ambayo inaingiliana na mhimili wa nne wa nadharia ya Usomi Tendaji ya Bruner (1966) unaosisitiza kuwa, mchakato wa ujifunzaji huwa bora zaidi wanafunzi wakijumuishwa kwani wao hujenga maana pamoja na hivyo basi, kuimarishana kiujuzi.

Katika darasa jumuishi, mwanafunzi aliye na ulemavu hujitambulisha na mwalimu aliye na ulemavu anapokuwa akitoa mafunzo na kuwaongoza wanafunzi masomoni. Katika madarasa jumuishi, mwalimu aliye na ulemavu huwatayarisha wanafunzi walio na wasio na ulemavu katika ulimwengu wao wa nje (Storey, 2007). Maoni ya Storey (2007) yanashadidiwa na Hauk (2009) ambaye anadai kuwa, walimu wenye ulemavu

huwa na nafasi muhimu katika kuwa mfano mzuri wa kuigwa na wanafunzi wote na vilevile kuleta sifa za kipekee darasani ikiwemo kukumbatia elimu jumuishi na mbinu bunifu za ufunzaji. Aidha, kwa mujibu wa Lewis na wenzake (2003), kwa miaka mingi watu wengi wenye ulemavu wa macho (upungufu wa macho na upofu kamili) wamefanikiwa kuwa walimu bora wa wanafunzi wenye ulemavu wa macho.

Kutokana na wataalam hawa, yaani Storey (2007) na Hauk (2009) tunaweza kusema kuwa wanafunzi wote darasani, yaani walio na wasio na ulemavu wa macho huwa na uhusiano mzuri na mwalimu mwenye ulemavu wa macho katika mchakato mzima wa ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, ingawa mwalimu huyu alikuwa na uhusiano mzuri na wanafunzi wote darasani katika ufunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili, ilibainika wazi kutokana na uchunguzi kuwa kulikuwa na changamoto katika kufundisha baadhi ya stadi za lugha kama vile, stadi ya kuandika na kusoma na hili lilitokana na kutokuwepo kwa matini na vifaa maalum vya kufundishia. Tofauti na shule jumuishi ya Menengai ambayo mtafiti alibaini kuwepo kwa mwalimu aliye na ulemavu wa macho, shule jumuishi ya msingi ya Joel Omino haikuwa na mwalimu wa aina hiyo.

3.2 Tofauti ya Ushirikiano wa Wazazi kati ya Shule ya Menengai na Joel Omino

Ushirikiano wa wazazi unaelezewa kama sehemu tendaji ya wazazi ya kujihusisha katika ukuaji na ujifunzaji wa wanafunzi wao shuleni na kuhakikisha kuwa wana uelewa zaidi kuhusu maisha ya wanafunzi wao shuleni (Williams na wenzake, 2002). Wataalam wengi wa elimu maalum huchukulia kuwahusisha wazazi katika mchakato wa ujifunzaji kama kipengele muhimu cha kuwapa elimu bora watoto wenye ulemavu

(Hornby, 1995; Seligman, 2000). Hata hivyo, hili halifanyiki wakati wote kwani kuna uwezekano wa mvutano kati ya shule na wazazi wa wanafunzi wenye ulemavu wa macho (Seligman, 2000). Utafiti huu ulithibitisha kuwa katika shule jumuishi ya Joel Omino ushirikiano wa wazazi na shule ulikuwa wa kiwango cha chini ikilinganishwa na shule jumuishi ya msingi ya Menengai.

Katika shule ya Joel Omino kutokana na usaili uliofanywa na walimu na vilevile, hojaji zilizojazwa na wanafunzi teule ilibainika kuwa wazazi wengi wa wanafunzi wenye ulemavu wa macho walitoka katika vitongoji duni vya Nyalenda. Kutokana na hali duni ya maisha, hawakuwa na uelewa au uwezo unaohitajika kuwashughulikia wanafunzi hawa. Kulingana na Mwakyeja (2013) wanafunzi wenye ulemavu wa macho wanaotoka sehemu iliyo nyuma kijamii na kiuchumi katika jamii kwa kawaida huwa na uwezo wa chini wa kujipatia rasilimali, kwani hawana njia maalum ya kupata mapato. Wazazi walio sehemu ya jamii hizi kwa kawaida hawana elimu, ujuzi na uwezo wa kuboresha ujifunzaji kati ya wanafunzi wao wenye ulemavu wa macho. Wanapokosa kutoa vifaa vya kuboresha ujifunzaji, teknolojia na vifaa vingine, hivyo basi wanafunzi wenye ulemavu wa macho hupata changamoto kuboresha ujifunzaji wao.

Asilimia kubwa ya wazazi kulingana na baadhi ya walimu hasa mwalimu aliye na mafunzo ya kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho hawana ushirikiano bora na shule hiyo katika kuwasaidia wanafunzi wao katika ujifunzaji.

Mwalimu huyu alisema kuwa;


Baadhi ya wazazi hawakubali wanapoambiwa kuwa watoto wao wana ulemavu wa macho kutokana na mtazamo hasi walio nao. Mtazamo huu hutokana na kukosa ujuzi na uelewa wa hali hii. Hili huwapelekea kutonunua vifaa vinavyohitajika katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kama vile miwani na vitabu vilivyo na nafasi kubwa ya kuandikia kati ya mistari.

Katika shule ya Menengai hali ilikuwa tofauti kwani kulingana na walimu waliohojiwa ilidhihirika kuwa asilimia kubwa ya wazazi wa wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule hii walishirikiana na walimu ili watoto wao wapate masomo bora. Delgado-Gaitan (1991) anasema kuwa, walimu wanatarajia wazazi kushiriki katika masomo ya watoto wao kwa kuwasiliana na shule ambapo watoto wao wanasomea na kuwasaidia katika masomo yao nyumbani. Ili wajihusishe ipasavyo katika shughuli za shuleni, wazazi wanafaa kujifahamisha kuhusu mfumo wa shule na utaratibu wake. Walimu hawa walisema kuwa wazazi walipoitwa shuleni ili kufuatilia masomo ya watoto wao walishirikiana ipasavyo. Vilevile, iwapo walihitajika kununua vifaa fulani ambavyo vingewasaidia wanafunzi wao walifanya hivyo. Hata hivyo, kulingana na mwalimu mmoja, wazazi ambao hawakuweza kujimudu walisaidiwa na wasimamizi na wafadhili tofauti.

3.3 Tofauti ya Tajiriba ya Walimu kati ya Shule Jumuishi Lengwa

Katika shule ya Menengai, walimu wanne kati ya watano wanaofunza somo la Kiswahili hawakuwa na ujuzi wa kuwashughulikia wanafunzi walio na ulemavu wa macho. Mwalimu mmoja tu ndiye alikuwa amemaliza kozi husika ya kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho na alishughulikia darasa la nne peke yake. Kando na asilimia kubwa ya walimu wa Kiswahili kukosa ujuzi, ilibainika kutokana na

mahojiano kuwa hawakuwa na tajiriba ya kutosha ya kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Grafu 3.1 inaonyesha miezi au miaka ambayo walimu wanaofunza somo la Kiswahili wamewashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi ya Menengai.




Grafu 3.1: Tajiriba ya Ufunzaji katika Shule ya Menengai

Kutokana na grafu 3.1 shule ya Menengai ilikuwa na walimu watano wanaoshughulikia madarasa ambayo wanafunzi wenye ulemavu wa macho wanapatikana. Majina yote yaliyotumika ni ya lakabu. Mwalimu Amina amefunza katika shule hii jumuishi kwa miezi minne peke yake, mwalimu Juma amefunza Kiswahili katika shule hii kwa muda wa miaka mitatu, mwalimu Zawadi kwa miaka miwili, mwalimu Aisha kwa miaka mitatu na hatimaye mwalimu Aziza kwa miaka mitano. Ilibainika kuwa mwalimu Amina ambaye alikuwa na mafunzo ya kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho alikuwa na tajiriba ya chini zaidi, yaani miezi minne peke yake. Ilhali walimu hao wengine wanne hata kama walikuwa na ujuzi wa kiwango cha juu ikilinganishwa

na mwalimu Amina, hawakuwa na mafunzo maalum ya kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho na hili liliathiri ufunzaji wao wa stadi za lugha ya Kiswahili hasa kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho kulingana nao.

Tofauti na shule ya Menengai shule ya Joel Omino ilikuwa na walimu wanne wanaowashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho walio na tajiriba ya juu zaidi kulingana na mahojiano na walimu katika shule lengwa. Grafu 3.2 inaonyesha miezi au miaka ambayo walimu wanaofunza somo la Kiswahili wamewashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi ya Joel Omino.



Grafu 3.2: Tajiriba ya Ufunzaji katika Shule ya Joel Omino

Kutokana na grafu 3.2 shule ya Joel Omino ilikuwa na walimu watano wanaowashughulikia madarasa ambayo wanafunzi wenye ulemavu wa macho wanapatikana kama hali ilivyo katika shule ya Menengai. Aidha, sawa na shule ya Menengai walimu wanne kati ya watano wanaofunza somo la Kiswahili hawakuwa na ujuzi wa kuwashughulikia wanafunzi walio na ulemavu wa macho. Walimu watatu walikuwa na tajiriba ya zaidi ya miaka mitano ilhali walimu wawili walikuwa na

tajiriba ya miaka minne na miezi minne mtawaliwa. Mwalimu Waridi amefunza katika shule hii jumuiishi kwa miezi minne peke yake, mwalimu Baraka amefunza Kiswahili katika shule hii kwa muda wa miaka minne, mwalimu Nuru kwa miaka minane, mwalimu Ali kwa miaka kumi na tisa na hatimaye mwalimu Neema kwa miaka kumi.

Ilidhihirika kuwa mwalimu Ali ambaye alikuwa na mafunzo ya kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho pia ndiye alikuwa na tajiriba ya juu zaidi ya miaka kumi na tisa. Bila shaka, walimu katika shule ya Joel Omino wakilinganishwa na wale wa shule ya Menengai walikuwa na tajiriba ya juu zaidi katika kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Kwa mujibu wa Lamichhane (2017), tajiriba ya kufunza ina uhusiano wa karibu na uamuzi wa kurekebisha mtindo wa kufunza ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Kadri ambavyo miaka ya kufundisha inavyoendelea, kuna uwezekano mkubwa wa walimu kubadilisha mtindo wao wa kufundisha na hivyo basi, kuwa mwalimu bora.

3.4 Tofauti ya Upatikanaji wa Chumba Maalum katika Shule Lengwa

Tofauti nyingine ya kimazingira iliyojitokeza katika shule lengwa ilikuwa ni upatikanaji wa chumba maalum. O'brien (1973) anaeleza chumba maalum kuwa chumba ambacho kina wafanyakazi na vifaa maalum ambapo wanafunzi wenye upungufu wa kuona na wenye upofu kamili wanaosoma katika madarasa ya kawaida huja kwa vipindi vya kawaida kila siku kwa mafunzo ya kibinafsi katika stadi maalum au kadri ambavyo mahitaji yanajitokeza. Katika shule ya Menengai kulikuwa na chumba maalum ambacho kilitumiwa na wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Uchunzaji ulidhihirisha

kuwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho walikutana hapa ili kupata mafunzo zaidi ya somo la Kiswahili kufidia yale ambayo mwalimu alishughulikia katika darasa jumuishi.

Aidha, katika chumba hiki kulikuwa na msomaji wa breli, mashine za breli na walimu ambao wana mafunzo ya kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Chumba hiki kutokana na mahojiano na walimu wanaofunza somo la Kiswahili, kina baadhi ya nyenzo zinazohitajika katika ujifunzaji wa stadi za Kiswahili kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Mwalimu Amina ambaye ana mafunzo ya kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho ndiye huwasaidia wanafunzi katika chumba hiki na alikuwa na haya ya kusema;

Hata kama vitabu vilivyo katika maandishi makubwa na vilevile, vilivyochapishwa kwa breli havipo, wanafunzi wenye ulemavu wa macho hunufaika na baadhi ya vifaa vya ujifunzaji ambavyo vipo katika chumba hiki maalum ili kuboresha stadi zao za lugha. Mathalan, vifaa halisi, modeli za kufundishia, michoro na picha ambazo zimekuzwa huhifadhiwa katika chumba hiki. Aidha, chati zenye rangi tofauti ambazo hutumiwa kwa wanafunzi walio na upungufu wa kuona hupatikana humu ikiwemo vifaa vya kidijitali kama vile rununu zenye sauti ambavyo hutumiwa na wanafunzi wenye upofu kamili. Muda fulani hutengewa wanafunzi wenye ulemavu wa macho ili waweze kutangamana na walimu wenye mafunzo maalum ya kuwashughulikia nje ya madarasa yao ya kawaida na vilevile, kutangamana na vifaa vya kufundishia katika chumba hiki maalum ili kuboresha ujifunzaji wao wa stadi za Kiswahili.

Ni bayana kuwa, chumba maalum ni chumba muhimu katika kunasa hisia na kuteka ari ya mwanafunzi kutaka kujifunza zaidi kwani vifaa vya ujifunzaji na vilevile, walimu walio na ujuzi wa kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho wanapatikana hapa kama inavyodhihirishwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya Usomi Tendaji ya Bruner (1966) unaoshikilia kuwa, wanafunzi huunda maana yao wenyewe. Kujifunza

lazima kuanze na masuala ambayo yanapatikana katika mazingira ya wanafunzi ambayo wanajaribu kikamilifu kuunda maana. Walimu wanafaa kutengeneza mazingira bora yatakayotumiwa katika ujifunzaji.

Kulingana na Sherpa na Baraily (2021) huduma zinazopatikana katika chumba maalum huziba pengo kati ya mwanafunzi na elimu jumuishi katika kutoa stadi za kimsingi kama vile matumizi ya breli na lugha ya ishara. Al-Zoubii na Rahmanii (2012) wanaakisi maoni ya Sherpa na Baraily (2021) kwa kusema kuwa, chumba maalum kifaacho huimarisha stadi ya kusoma, kuandika ikiwemo stadi nyinginezo. Wanaendelea kusema kuwa, wanafunzi walio na uzoefu wa kutumia chumba hiki wana uwezo wa kufikia umahiri wa stadi za kimsingi katika umri mdogo.

Kinyume na shule ya Menengai, matokeo ya uchunzaji na mahojiano na walimu na wanafunzi katika shule ya Joel Omino yalidhihirisha kuwa hakukuwa na chumba maalum. Aidha, nyenzo za kufundishia somo la Kiswahili zilikuwa haba ikilinganishwa na shule ya Menengai. Mwalimu Ali alidokeza kuwa;

Mwanafunzi mwenye ulemavu wa macho hapewi msaada maalum nje ya darasa baada ya somo kwani hakuna chumba maalum. Aidha, nyenzo za kufundishia stadi za lugha ya Kiswahili ambazo zinapatikana hapa hazikidhi mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho ifaavyo kwani ni chache. Nyenzo zinazopatikana hapa kwa urahisi ni chati za rangi ambazo zimeandikwa katika maandishi makubwa.


Wanafunzi wenye ulemavu wa macho waliohojiwa walieleza kuwa nyenzo za kufundishia na vifaa vya kidijitali havikutumika kwa kiasi kikubwa wakati wa somo la Kiswahili darasani.

Chati 3.1 inaonyesha jamii lugha za kwanza za wanafunzi katika shule ya Menengai.

Mtafiti alibaini kuwa kati ya wanafunzi tisa walio na ulemavu wa macho katika shule ya

Menengai wanafunzi watano walizungumza lugha ya Kikuyu, mmoja lugha ya Dholuo, mmoja lugha ya Ekegusii na watatu lugha ya Kiluhya. Kwa jumla, majibu ya hojaji yalionyesha kuwa wanafunzi katika madarasa mbalimbali katika shule ya Menengai wanatoka mazingira ya wingi lugha. Wanafunzi ni wakazi wa mitaa mbalimbali mjini Nakuru kama vile, Mawanga, Rhonda, Free Area, Bondeni, Kabachia, Barnabas, Heshima, Kivumbini, Kiti na kadhalika. Mitaa hii huwa na athari fulani katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa sababu lugha za kwanza huathiri umilisi wa lugha ya pili katika viwango mbalimbali. Aidha, ilifahamika kuwa lugha ya Sheng' hutumika kwa kiasi kikubwa katika mitaa hii.

Kwa upande mwingine, usuli wa lugha katika shule ya Joel Omino ulikuwa tofauti ikilinganishwa na mazingira ya shule ya Menengai kwani lugha asili zinazozungumzwa na wanafunzi wengi ni Dholuo, Ekegusii na Kiluhya. Chati 3.2 inaonyesha majibu ya wanafunzi mia moja na watano waliojaza hojaji (walio na wasio na ulemavu wa macho):



Chati 3.2: Lugha za Asili za Wanafunzi wa Shule ya Joel Omino

Chati 3.2 inaonyesha jamii lugha zinazopatikana katika shule ya Joel Omino. Wanafunzi wote wanane walio na ulemavu wa macho katika shule hii, walizungumza lugha ya Dholuo. Aidha, wanafunzi mia moja na wawili kati ya wanafunzi mia moja na watano walitoka katika vitongoji duni vya Nyalenda ambavyo lugha kuu inayotumika ni lugha ya Dholuo.

Chati 3.1, ilidhihirisha kuwa shule ya Menengai iko katika mazingira ya wingi lugha na wanafunzi wengi wana usuli wa lugha za Kibantu (78%) ilhali wanafunzi wengi katika shule ya Joel Omino wanazungumza lugha ya Dholuo (92%) kulingana na chati 3.2. Usuli huu unachangia pakubwa katika changamoto ambazo wanafunzi wenye ulemavu wa macho wanapata katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili. Lugha za Kibantu zina ukuruba wa kimuundo na Kiswahili, jambo ambalo linaweza kuwa na athari chanya ilhali Dholuo ni lugha ya Kinailoti ambayo muundo wake unatofautiana sana na

Kiswahili. Hivyo basi, ni rahisi zaidi kwa wanafunzi kujiundia maana katika shule ya Menengai kutokana na usuli wa lugha nyingi za Kibantu kuliko ilivyo katika shule ya Joel Omino. Kwa upande mwingine, kiwango cha juu cha matumizi ya Sheng' kinaweza kuwa kikwazo katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa sababu uzoefu wa Sheng' unawafanya wanafunzi kutobainisha tofauti kati ya Sheng' na Kiswahili sanifu. Changamoto ambayo si kubwa katika shule ya Joel Omino.

Matokeo yanaonyesha tofauti iliyoko katika usuli wa lugha kati ya wanafunzi wa shule ya Menengai na Joel Omino. Kutokana na hali hii, kuna athari tofauti katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi hawa kutokana na mazingira yao inavyoelekezwa na mhimili wa kwanza wa nadharia ya kujifunza ya Usomi Tendaji inayoshikilia kuwa, wanafunzi huunda maana yao wenyewe. Kwa hivyo, kujifunza lazima kuanze na masuala ambayo yanapatikana katika mazingira ya wanafunzi ambayo wanajaribu kikamilifu kuunda maana.

3.6 Hitimisho

Sura hii imejikita katika kuchanganua na kuwasilisha data kuhusu tofauti za usuli wa mazingira ya ujifunzaji kati ya shule jumuishi ya Menengai na Joel Omino. Mtafiti alitambua tofauti tano za kimazingira kati ya shule mbili zilizolengwa katika uchunguzi huu kwa kutumikiza mihimili miwili ya nadharia ya Usomi Tendaji ya Bruner (1966). Sura inayofuata imeshughulikia uchanganuzi na uwasilishaji wa data ya athari za tofauti za kimazingira kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili.

SURA YA NNE

ATHARI ZA TOFAUTI ZA KIMAZINGIRA KWA WANAFUNZI WENYE ULEMAVU WA MACHO KATIKA UJIFUNZAJI WA STADI ZA LUGHA YA KISWAHILI

4.0 Utangulizi

Sura ya tatu imeshughulikia tofauti za usuli wa mazingira ya ujifunzaji kati ya shule jumuishi ya Menengai na Joel Omino. Sura hii imehusisha uchanganuzi wa data ya athari za tofauti za kimazingira kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili. Data hii ilichanganuliwa kwa kutumia mhimili wa kwanza wa nadharia ya Usomi Tendaji ya Bruner (1966) unaoshikilia kuwa wanafunzi huunda maana yao wenyewe. Kwa hivyo, kujifunza lazima kuanze na masuala ambayo yanapatikana katika mazingira ya wanafunzi ambayo wanajaribu kikamilifu kujiundia maana. Mazingira ya ujifunzaji yana jukumu muhimu katika ujifunzaji wa stadi za lugha kwa wanafunzi wote na hasa kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho. Kutokana na uchanganuzi wa data, mtafiti alibaini athari za mazingira kufanana na kutofautiana katika shule lengwa.

4.1 Athari ya Mazingira ya Kelele

Mazingira ya darasani kama vile idadi kubwa ya wanafunzi madarasani na eneo ambalo shule inapatikana huwa na athari katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili. Vipengele hivi viwili huamua kiwango cha kelele katika mazingira ya ujifunzaji. Kiwango cha kelele katika mazingira ya darasani huwa na athari katika kiwango ambacho wanafunzi wenye ulemavu wa macho watakuwa makini darasani na umakini

huu, huwa na nafasi kubwa katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili. Lane (2008) akichangia kuhusu umuhimu wa umakini katika ujifunzaji wa stadi za lugha anaeleza kuwa tafiti nyingi zimeripoti uhusiano kati ya ulemavu wa macho na matatizo ya kuwa makini katika stadi ya kusoma. Kulingana naye, wakati ambapo mwendo wa kusoma wa wanafunzi walio na ulemavu wa macho haufanani na ule wa wanafunzi wenzao wasio na ulemavu wa macho, wanafunzi hawa huwa katika hatari ya matatizo ya kielimu.

Kipengele cha eneo ambapo shule inapatikana kina athari katika kiwango cha umakini ambacho mwanafunzi atakuwa nacho darasani. Kinyume na shule ya Joel Omino inayopatikana nje ya mji wa Kisumu, shule ya Menengai iko katika mazingira ya mjini. Matokeo ya uchunzaji na mahojiano na walimu yalidhihirisha kuwa eneo la shule ya Menengai lina kelele wakati wa ujifunzaji kwani shule hii iko katikati ya barabara mbili kuu ambapo magari hupita na wakati mwingine treni. Suala hili linaathiri ujifunzaji wa stadi ya kusikiliza na hivyo basi, ujifunzaji wa stadi zingine huathirika pia kutokana na mwingiliano wa stadi hizo. Hii inatokana na kuwa kusikiliza ni muhimu sana kwa mtu yeyote aliye na shida ya kuona kwa sababu kelele zinaweza kuathiri umakini na utambuzi wao. Kutokana na haya ilibainika kuwa, wanafunzi wa shule ya Menengai wanaathirika zaidi katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na wale wa shule ya Joel Omino.

Kando na kipengele cha eneo ambapo shule inapatikana, kipengele cha idadi ya wanafunzi madarasani vilevile kinaathiri kiwango cha umakini ambacho mwanafunzi

atakuwa nacho darasani. Matokeo ya mahojiano na uchunzaji yalionyesha kuwa shule za Menengai na Joel Omino zilikuwa na mazingira ambayo hayakuboresha ujifunzaji wa stadi za lugha. Kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi katika madarasa yaliyotafitiwa katika shule zote mbili, kulikuwa na athari ya kelele kwa sababu ni vigumu kwa mwalimu kudhibiti darasa kubwa kiasi hicho. Jambo hili liliathiri umakini katika ufunzaji na ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili, mathalan, kusoma na kuandika. Hali hii inakinzana na maoni ya Webster na Roe (1998) wanaoshikilia kuwa kiwango cha sauti katika mazingira ni muhimu kwani wanafunzi walio na ulemavu wa macho huhitaji kutumia habari wanazozipata kupitia stadi ya kusikiliza. Hali tulivu ya mazingira inayoboresha usikilizaji na isiyo na vyanzo vya sauti vinavyoshindana ni muhimu. Shield na Dockrell (2008) wanashadidia maoni ya Webster na Roe (1998) kwa kusema kuwa, kelele huwa na athari hasi katika ujifunzaji na utendaji wa watoto.

Rost (2002) alitambua kuwa, stadi ya kusikiliza ndiyo stadi ya kwanza tunayoshiriki wakati tunapozaliwa. Stadi hii ndiyo uti wa mgongo wa upataji na maendeleo ya lugha. Stadi ya kusikiliza ni kipengele muhimu cha upataji wa lugha ya kwanza na kwa vyovyote vile ni muhimu sana katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Bamba (2012) anadai kuwa, kufundisha stadi ya kusikiliza katika madarasa yaliyo na idadi kubwa ya wanafunzi, ambapo uwiano wa mwanafunzi kwa mwalimu ni 40: 1 au 50: 1, kunaweza kuwa jambo gumu sana. Kulingana naye, madarasa yaliyo na idadi kubwa ya wanafunzi yana sifa ya kuwa na matatizo ya kawaida ikiwa ni pamoja na nidhamu ya wanafunzi, kujihusisha katika mchakato wa ujifunzaji, matatizo ya kutathmini ujuzi wa wanafunzi wote na kuwapa matokeo.

Haya yanadhihirika kutokana na mahojiano na mwalimu Amina anayefunza shule ya Menengai aliyesema kuwa;

Idadi kubwa ya wanafunzi darasani inaweza kupelekea kuwepo kwa kelele na hili huwa na athari hasi katika stadi ya kusikiliza. Stadi ya kusikiliza ikiathiriwa mara nyingi huchangia wanafunzi kutokuwa makini katika mchakato mzima wa ujifunzaji. Wanafunzi hasa walio na ulemavu wa macho hutegemea stadi hii ili waweze kukuza stadi zingine za lugha. Mara nyingi, wanafunzi hawa huhisi kwamba wamepuuzwa katika madarasa haya na hivyo basi, kupoteza ari ya kujifunza.

Uchunzaji ulionyesha kuwa idadi kubwa ya wanafunzi katika shule zote mbili iliwafanya wanafunzi kutumia nafasi yoyote kuzungumza wao kwa wao huku mwalimu akifunza. Ilimbidi mwalimu awaombe wanafunzi mara kwa mara wanyamaze ili wafuatilie somo. Hili lilitatiza mchakato wa ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili hasa kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Matokeo haya yanalingana na maoni ya Nolan na Morris (1973) wanaosema kuwa, pembejeo ya kusikia ni njia mojawapo ambayo wanafunzi walio na ulemavu wa macho hujifunza na kupata maarifa. Stadi ya kusikiliza imeonekana kuwa bora zaidi kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho ikilinganishwa na stadi ya kusoma. Katika mazingira yoyote ya kielimu, ustadi mzuri wa kusikiliza huwasaidia wanafunzi walio na ulemavu wa macho kufaulu katika stadi ya kusoma na mawasiliano kupitia kuandika na kuzungumza (Heward, 2000).

Aidha, uchunzaji pia ulidhihirisha kuwa idadi kubwa ya wanafunzi madarasani iliwazuia kuzunguka darasani kwa minajili ya kufuatilia na kuchunguza kile kila mwanafunzi alikuwa akifanya. Hii ni kutokana na madawati kuwa mengi hivi kwamba nafasi ya kupitia ilikuwa finyu sana. Hili lilitatiza mwingiliano baina ya mwanafunzi na

mwalimu. Kwa hivyo, kulikuwa na uwezekano wa wanafunzi katika shule mbili lengwa kukosa umakini na hivyo, kuacha kumsikiliza mwalimu.

4.2 Athari inayotokana na Hali ya Kiuchumi

Utafiti ulitambua kuwa kulikuwa na utofauti wa mazingira kati ya shule mbili lengwa katika hali ya kiuchumi. Shule ya Menengai inapatikana mjini ambapo kuna nafasi ya kutoa msaada wa ziada ikilinganishwa na shule ya Joel Omino ambapo wanafunzi wengi wanatoka katika vitongoji duni vya Nyalenda ambako rasilimali za elimu hazitoshi. Ilidhihirika kuwa, shule ya Menengai ilikuwa na chumba maalum ambacho kilikuwa na rasilimali muhimu katika ujifunzaji wa stadi za Kiswahili kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho. Tofauti na shule ya Menengai, shule ya Joel Omino kupitia uchunzaji na mahojiano na walimu na wanafunzi ilibainika kuwa haikuwa na chumba maalum na hivyo basi, kiwango cha vifaa vya ujifunzaji kilikuwa chini. Haya yalithibitishwa na mwalimu Nuru aliyedokeza kuwa;

Kazi nyingi wanazopewa wanafunzi wenye ulemavu wa macho huwa katika maadishi na mara nyingi vifaa vya ujifunzaji havitumiki kutokana na uhaba wao. Hili hutatiza umilisi wa lugha kupitia ujifunzaji wa stadi nne.

Kwa upande mwingine, mwanafunzi mmoja katika jopo alikiri kuwa;

Kando na kukosa vitabu vya kusoma vilivyo katika maandishi makubwa, vifaa vinginevyo havitumiki darasani na hivyo basi, ni vigumu kujifunza stadi ya kusoma na kuandika kwani ni vigumu kujua maendelezo ya maneno kutokana na kutofanya mazoezi katika stadi ya kusoma.

Kwa mujibu wa Vikoo (2003), darasa lisilo na vifaa vya ujifunzaji linaweza kusababisha matokeo duni kwa wanafunzi. Adetoro (2012) anadai kuwa tofauti na watu wasio na ulemavu wa macho, watu walio na ulemavu wa macho hupata maarifa kupitia

vifaa vya ujifunzaji kama vile breli, vitabu vya sauti, kinasa sauti na vitabu vilivyo katika maandishi makubwa. Hata hivyo kulingana naye, nyenzo hizi hazipatikani kwa idadi inayowafaa wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Matokeo ya utafiti wa Carasco (1996) yalithibitisha maoni ya Adetoro (2012) ambapo alibaini kuwa, mojawapo ya uzoefu mbaya darasani ni walimu kukosa kutumia vifaa vya ujifunzaji. Anaendelea kusema kuwa, walimu hawapewi vifaa ambavyo vingetumika kufunzia stadi ya kusoma.

Teknolojia za sauti ni vifaa vizuri vya ujifunzaji hasa kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho kwani vifaa hivi vinaweza kuwapa motisha, kuchochea shauku, kuhimiza maana na vilevile, vinaweza kutumika katika kutahini stadi ya kusikiliza (Barron, 2004; Parshall, 1999). Learning (2003) akichangia kuhusu vifaa vya ujifunzaji vinavyotumiwa na wanafunzi walio na ulemavu wa macho anasema kuwa, matumizi ya tarakilishi ni muhimu hasa kwa wanafunzi wenye matatizo ya kuona kwani uwezo wa kutumia kazi iliyo katika maandishi na kupata maarifa zaidi huboreshwa. Jukumu muhimu linalotekelezwa na matumizi ya vifaa hivi ni kuwasaidia wanafunzi kupata uhalisia wa dhana zilizo za kidhahania na hivyo basi, huwaruhusu wanafunzi kuwa na mwingiliano na maneno, ishara na mawazo kwa njia zinazokuza uwezo wao wa kusoma, kusikiliza, kuzungumza na kuandika (Njoroge, 2019; Bukoye, 2019).

Mwakyeja (2013) akiwarejelea Bishop (1996) na Mastropieri na Scruggs (2010) anaeleza kuwa ili kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu wa macho, nyenzo za kufundishia zinafaa kurekebisha ili zikidhi mahitaji yao. Kwa mfano, maandishi

yaliyochapishwa yanaweza kurekebisha kwa kuongeza ukubwa wa fonti, kuweka maandishi katika herufi kubwa, kuongeza rangi na kurekebisha nafasi kati ya maneno. Walakini, kiwango cha urekebishaji huu kinategemea kiwango cha kuona na mahitaji ya mwanafunzi anayehusika. Walimu wanafaa kufahamu kuwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho wana upungufu katika uelewa wa dhana kutokana na upungufu wa uwezo wa kuona, hivyo basi urekebishaji wa nyenzo za kufundishia ni muhimu ikiwa wanahitajika wajifunze yale yote ambayo wanafunzi wasio na ulemavu wa macho wanajifunza darasani. Katika shule ya Menengai haya yalidhihirika kutokana na mahojiano na mwalimu Aisha aliyesema kuwa;

Hata ingawa muda hautoshi wa kutayarisha vifaa vya ujifunzaji vya wanafunzi walio na ulemavu wa macho mara nyingi mimi humshirikisha mwalimu aliye na ujuzi wa kushughulikia wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika kutayarisha vifaa vitakavyotumika darasani na iwapo haitawezekana, muda hutengwa ili wapate kutumia vifaa hivi katika chumba maalum. Kwa mfano, ili kuboresha mwendo wa kusoma wa wanafunzi hawa, vifaa vya kusikiliza hutumiwa. Vifaa hivi huboresha ujifunzaji wa msamiati na sarufi kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho.

Kinyume na maoni ya mwalimu Aisha matokeo ya uchunzaji katika shule hii, yalithibitisha kuwa walimu hawakutumia vifaa vya ujifunzaji darasani kama vile chati, ubao na vinginevyo. Walitumia mbinu ya kuhadhiri peke yake na kisha kuwapa wanafunzi kazi ya ziada. Hivyo basi, ujifunzaji wa wanafunzi walio na ulemavu wa macho haukuboreshwa darasani na iliwabidi kupata masomo ya ziada katika chumba maalum. Hata hivyo, ni vigumu mwalimu aliye katika chumba hiki kumshughulikia kila mwanafunzi.

Aidha, kando na hali ya kiuchumi ya shule ya Joel Omino ambapo chumba maalum kilikosekana, vilevile ilikuwa vigumu kwa wazazi kumudu kununua ala za macho ambazo ni ghali na vilevile kununua vifaa vya kusoma vilivyo vya bei ya juu kutokana na kipato cha chini cha wakazi wa vitongoji vya Nyalenda ikilinganishwa na wazazi wa shule ya Menengai ambao wengi wao walimudu kununua baadhi ya vifaa ambavyo vilikuwa vinahitajika na wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Matokeo ya utafiti huu yanadhihirisha kuwa, kuna uwezekano wa wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule ya Joel Omino kukosa kujifunza stadi za lugha ya Kiswahili ifaavyo ikilinganishwa na wanafunzi katika shule ya Menengai kutokana na hali yao ya kiuchumi.

4.3 Athari ya Usuli wa Lugha

Kulingana na Careless (2008), lugha ya asili ina athari chanya na hasi katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Atkinson (1993) anadai kuwa, lugha ya asili inaweza kuwa na ‘hatari kubwa zaidi’ katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Maoni ya Careless (2008) na Atkinson (1993) yanaoana na yale ya Beardsmore (1982) ambaye anasema kuwa, matatizo mengi anayopata mwanafunzi katika kujifunza lugha ya pili katika fonolojia, msamiati na sarufi yanatokana na athari ya lugha ya kwanza. Katika shule ya Joel Omino mtafiti alitambua kuwa, wanafunzi walio na ulemavu wa macho hawakujifunza stadi ya kuandika na kuzungumza ifaavyo ikilinganishwa na wenzao katika shule ya Menengai. Hii ilitokana na athari ya tofauti ya usuli wa lugha kutokana na mazingira yao tofauti. Wakati ambapo mazingira ya ujifunzaji yana athari, matumizi ya mhimili wa kwanza wa nadharia ya Usomi Tendaji (Bruner, 1966) unaoshikilia kuwa, kujifunza lazima

kuanze na masuala ambayo yanapatikana katika mazingira ya wanafunzi ambao wanajaribu kikamilifu kuunda maana yanabainika.

Kulingana na Bhela (1999) wakati wa kuandika au kuzungumza lugha ya pili, wanafunzi wanaojifunza lugha hii mara nyingi hutegemea mifumo ya lugha yao ya asili ili kupitisha mawazo yao. Ilidhihirika kutokana na hojaji zilizojazwa na wanafunzi kwamba, wanafunzi wote walio na ulemavu wa macho katika shule ya Joel Omino walizungumza lugha ya asili ya Dholuo ilhali katika shule ya Menengai asilimia sabini na nane ya wanafunzi wana usuli wa lugha za Kibantu. Athari ilionekana katika viwango tofauti vya kiisimu. Viwango hivyo ni kama vile; uambishaji na ngeli, idadi ya fonimu, mofolojia na sintaksia. Utafiti huu utaeleza viwango hivi moja baada ya kingine.

4.3.1 Uambishaji na Ngeli

Lugha za Kinailoti mathalan Dholuo hasa katika mchakato wa kuambisha nomino katika hali ya wingi huwa tofauti na lugha za Kibantu. Kuna mabadiliko mbalimbali ya udondoshaji wa irabu, uchopekaji, ubadilishaji wa konsonanti za wingi na urekebishaji wa sifa ya irabu (Adicka, 2016). Hili hudhihirisha ukinzano katika uambishaji wa nomino za Kibantu katika hali ya wingi ambapo huchukua viambishi vya wingi bila mabadiliko yoyote.

Kutokana na mahojiano na walimu na wanafunzi wa Joel Omino ilithibitishwa kuwa lugha ya kwanza ilikuwa na athari hasi katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi hasa wanafunzi wenye ulemavu wa macho ambao kwa kiasi kikubwa

huwategemea wenzao wasio na ulemavu wa macho katika kujifunza. Mwalimu Ali alidai kwamba;

Athari hasi inayoonekana katika ujifunzaji wa stadi zote nne za lugha huchangiwa na mazingira ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Wanafunzi wengi wana mazoea ya kutumia lugha yao ya asili wanapotangamana na familia zao na marafiki wao katika mazingira yao ya nyumbani na shuleni. Kando na kuzungumza lugha isiyo sanifu athari pia huonekana katika stadi ya kuandika ambapo makosa mengi ya kisarufi hasa katika uandishi wa insha hujitokeza. Wanafunzi wengi huwa na matatizo katika maendeleo ya maneno na vilevile, katika matumizi ya ngeli. Kwa mfano, utapata mwanafunzi amendika kuwa, 'kijiko changu ulianguka chini.'

Maoni ya Ali yanaingiliana na maoni ya Setti (2016) anayesema kuwa, miongoni mwa stadi nne za lugha; stadi ya kuandika inachukuliwa kuwa stadi ngumu zaidi kupata. Karim na Nassaji (2013) wanashadidia maoni ya Setti (2016) kwa kusema kuwa, wanafunzi wanapoandika katika lugha ya pili, lugha yao ya asili huwa na athari katika uandishi wao. Mahojiano katika majopo na wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule ya Joel Omino yalidhihirisha kuwa walipata shida katika stadi ya kuandika kwani matumizi ya ngeli yaliwatatiza. Vilevile, katika stadi ya kuzungumza ilikuwa vigumu kuzungumza Kiswahili sanifu. Uchunzaji ulionyesha kuwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho walipata changamoto kujieleza katika lugha ya Kiswahili na walichagua kujieleza kwa kutumia lugha ya Kiingereza hasa walipokuwa wakihojiwa.

Hata hivyo, walimu wa Kiswahili walipohojiwa kuhusu changamoto hizi zilizotambuliwa kutokana na kushiriki katika mahojiano na wanafunzi wenye ulemavu wa macho walisema kuwa walikuwa wameweka mikakati ili kuwahimiza wanafunzi kuboresha stadi yao ya kuzungumza na hivyo basi, kuboresha pia stadi ya uandishi.

Mojawapo ya mikakati hii ni kama vile wanafunzi kuwasiliana kwa kutumia lugha ya Kiswahili siku ya Ijumaa ikilinganishwa na siku zingine ambazo wao hutumia lugha ya Kiingereza na wanafunzi wanaopatwa wakizungumza kwa kutumia lugha yao ya asili huadhibiwa.

Hali ilikuwa tofauti katika shule ya Menengai kwani asilimia kubwa ya wanafunzi (78%) wanazungumza lugha za Kibantu. Kwa mujibu wa Adicka (2016) sawa na lugha zingine za Kibantu, nomino za Kiswahili huwekwa katika makundi (ngeli) kwa kuzingatia vigezo vya kisemantiki, kimofolojia na kisintaksia. Uanishaji wa nomino za Kiswahili ni tofauti na ilivyo katika mfumo wa lugha ya Dholuo kwa vile Kiswahili ni lugha ya Kibantu nayo Dholuo ni lugha ya Kinailoti. Nomino za Dholuo hazina makundi yanayotokana na viambishi awali vya nomino zenyewe.

4.3.2 Idadi ya Fonimu

Lugha ya Kiswahili na Dholuo hutofautiana katika msingi wa fonimu zinazopatikana katika kila lugha. Hii inamaanisha kuwa, kuna konsonanti zinazopatikana katika lugha moja na si nyingine. Lugha ya Dholuo ina idadi ya konsonanti ishirini na sita sawa na lugha ya Kiswahili. Walakini, kuna sauti za konsonanti katika lugha ya Kiswahili ambazo hazipatikani katika lugha ya Dholuo. Konsonanti hizi ni kama vile; /ʃ/, /ʒ/, /z/ na /v/ (Adicka, 2016).

Kutokana na tofauti hii wanafunzi wanaozungumza lugha ya asili ya Dholuo mathalani, walio katika shule ya Joel Omino hupata matatizo katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kama vile kuandika na kusoma kutokana na athari ya lugha ya asili

ikilinganishwa na wale ambao hawazungumzi lugha ya Dholuo. Kwa upande mwingine, wanafunzi katika shule ya Menengai ambao asilimia kubwa (78%) wanazungumza lugha za Kibantu, hawapati athari ya aina hii kwa kiasi kikubwa kwani Kiswahili ni lugha ya Kibantu pia.

4.3.3 Mofolojia

Pathan na Alsout (2014) wanashikilia kuwa, stadi ya kuzungumza inachukuliwa kuwa stadi muhimu zaidi kati ya stadi zingine kwani humwezesha mwanafunzi kuanzisha mawasiliano yenye mafanikio katika lugha husika, ambayo mara nyingi ndiyo lengo kuu la kujifunza lugha yoyote ya pili. Makosa ya kimatamshi na ya kisarufi ndiyo aina za kawaida za athari ya mwingiliano kati ya lugha ya asili na lugha ya pili wakati wa mazungumzo. Chanzo kikuu cha makosa katika stadi ya kuzungumza hutokana na mchakato wa kufikiria kwanza katika lugha ya asili au kutokana na kufanya tafsiri sisisi kutoka kwa miundo ya lugha asili na kisha kuwasilisha dhana katika lugha ya pili (Manrique, 2013; Subandowo, 2017). Kuhusu athari ya lugha ya Dholuo katika ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza mwalimu Waridi alisema kuwa;

Stadi inayoathiriwa sana kutokana na usuli wa lugha wa wanafunzi ni stadi ya kuzungumza. Matatizo hasa yanaonekana katika matumizi ya ngeli na katika kutamka maneno ya Kiswahili. Kwa mfano, utawapata wanafunzi wakisema 'Niongojee' badala ya 'Ningoje,' au 'Nisasema' badala ya 'nishasema.' Hili linatokana na wanafunzi kupendelea kutumia lugha yao ya asili katika mazungumzo ikilinganishwa na lugha ya Kiswahili hasa wanapokuwa peke yao katika vikundi nje na ndani ya darasa. Hili hutatiza juhudi ya kuboresha ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza.

Kinyume na lugha ya Dholuo ambayo utafiti ulibaini kuathiri upatanisho sahihi katika lugha ya Kiswahili, lugha za kibantu pia zilidhihirisha kutokuwa na athari yoyote kwa vile Kiswahili ni lugha ya Kibantu.

4.3.4 Sintaksia

Odlin (1989) anafafanua uhamishaji wa lugha kuwa athari inayotokana na maingiliano ya mifumo inayofanana na inayotofautiana kati ya lugha lengwa na lugha nyingine yoyote ambayo imepatwa hapo awali. Lado (1960) anasema kuwa, iwapo lugha zitakuwa na mifumo tofauti, kutakuwa na uhamishaji hasi, kwa sababu mwanafunzi atapata ugumu katika uzalishaji wa lugha. Dechert (1983) na Ellis (1997) wanakubaliana na mawazo ya Lado (1960) kwa kusema kuwa, ikiwa miundo ya lugha ya kwanza na lugha ya pili ni tofauti kabisa, basi inatarajiwa kutokea kwa makosa ya kiasi cha juu katika lugha ya pili. Tofauti na maoni ya Lado (1960), Gass na Selinker (2001) wanasema kuwa, lugha zinapokuwa na mifumo sawa, kutakuwa na uhamishaji chanya, kwa sababu lugha lengwa itawezeshwa na lugha ya asili. Maoni ya Gass na Selinker (2001) yanalingana na maoni ya Noor (1994) ambaye anadai kuwa, uhamisho unaweza kuwa chanya ikiwa stadi zozote za lugha ya asili zitawezesha ujifunzaji wa stadi za lugha ya pili kwa sababu ya usawa wa mifumo ya lugha hizi mbili.

Lugha ya Dholuo ni lugha ya Kinailoti yenye sifa ya kipekee (Achayo, 2003). Oduor na wenzake (2013) wakimrejelea Madara (1989) wanasema kuwa, katika lugha ya Dholuo viambishi vipatanishi lazima viwepo ikiwa kundi nomino limeundwa na kiwakilishi. Hata hivyo, kundi nomino likiundwa kwa nomino, viambishi vipatanishi huenda visiwepo. Jambo hili kulingana nao, ndilo huwafanya wanafunzi wengi

wanaozungumza lugha ya asili ya Dholuo kutatizika wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Aidha, kwa mujibu wa wataalam hawa, uhamishaji wa sarufi ya lugha ya Dholuo huathiri upatanishi wa kisarufi katika lugha ya Kiswahili kwa sababu kanuni za lugha hizi mbili ni tofauti. Athari hii hasi ilionekana wazi kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule ya Joel Omino hasa katika kiwango cha kiisimu cha sintaksia kutokana nao kuzungumza lugha ya asili ya Dholuo.

Tofauti na shule ya Joel Omino inayopatikana kijijini ambapo kwa kiasi kikubwa lugha ya Dholuo inatumika, shule ya Menengai inapatikana katika mazingira ya mjini yaliyo na sifa ya wingi lugha. Katika shule hii, utafiti ulibaini kuwa wanafunzi walioteuliwa walikuwa wanatumia lugha mseto za kiasili kutokana na wao kutoka katika jamii tofauti nchini Kenya. Hivyo basi, katika mawasiliano yao wanatumia lugha ya Kiingereza na Kiswahili kwa kiasi kikubwa.

Uchunzaji na mahojiano na wanafunzi walio na ulemavu wa macho na walimu zilionyesha kuwa Sheng' imeathiri ujifunzaji wa stadi ya kuandika na kuzungumza. Mekonge (2016) akiwarejelea Buliba na wenzake (2006) anasema kuwa, Sheng' hutokana na mwingiliano baina ya vijana wa makabila tofauti tofauti wanaoishi katika mitaa mbalimbali katika mji mmoja. Anaendelea kusema kuwa muundo wa Sheng' na Kiswahili hufanana. Hili hupelekea vijana kuchanganyikiwa wanapohitajika kutumia muundo wa Kiswahili sanifu katika kazi zao.

Momanyi (2009) anaunga mkono mawazo ya Mekonge (2016) kwa kusesitiza kuwa, Sheng' imejikita zaidi katika muundo wa Kiswahili na inatumia sarufi ya Kiswahili yenye leksimu inayotolewa katika lugha ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Momanyi (keshatajwa), Sheng' inatumika katika mazingira ya wingi lugha ya miji mikubwa kama vile, Nairobi, Nakuru, Kisumu, Eldoret na Mombasa. Maoni ya Mekonge (2016) na Momanyi (2009) yanashadidiwa na Githinji (2006) ambaye anashikilia kuwa, ushawishi wa makabila mbalimbali utaendelea kuwa na jukumu katika Sheng' kwa muda mrefu.

Walimu wote watano waliosailiwa walikiri kuwa, athari ya Sheng' ilijitokeza wazi kutokana na wanafunzi hawa kuwa wakazi wa mazingira ya mjini. Mwalimu Juma alidai kuwa;

Shuleni mikakati imewekwa ya kuhimiza matumizi ya Kiswahili sanifu. Hata hivyo, wanafunzi wanapokuwa katika mazingira ya nyumbani ambapo hakuna kanuni maalum zilizowekwa za kuhakikisha kuwa kuna matumizi mazuri ya lugha ya Kiswahili, kuna uwezekano wa kujihusisha katika matumizi ya lugha ya Sheng'. Athari ya lugha ya Sheng' huonekana wazi katika uandishi wa insha na vilevile, katika mazungumzo yao.

Mtafiti alitambua kutokana na uchunguzi wa wanafunzi walio na ulemavu wa macho walipokuwa wanahojiwa kuwa walipata shida kujieleza katika lugha ya Kiswahili kwani mara nyingi walibadili msimbo.

4.4 Athari ya Tajiriba ya Kufunza

Mtafiti alitambua kuwa tajiriba ya kufunza huwa na athari katika uwasilishaji wa somo darasani. Katika shule ya Menengai ilibainika kuwa, walimu wote

waliowashughulikia wanafunzi walio na ulemavu wa macho walikuwa na tajiriba ya chini ya miaka mitano. Ilhali katika shule ya Joel Omino mwalimu mmoja alikuwa na tajiriba ya kati ya miaka saba na kumi, wawili walikuwa na tajiriba ya zaidi ya miaka kumi ilhali wawili walikuwa na tajiriba ya kati ya miaka tatu na sita. Hii inaweza kuwa ni kutokana na kile Owoeye na Yara (2011) wakimrejelea Ibukun (1988) wanachosema, kuwa walimu hukataa kufanya kazi katika shule za kijijini ikilinganishwa na za mjini. Hivyo basi, ni vigumu walimu hawa wachache katika shule za kijijini kuhamishwa kutoka shule moja hadi nyingine ikilinganishwa na walimu wanaofunza katika shule za mjini. Hii ndio sababu kuu ya walimu wa mjini kuwa na tajiriba ya miaka michache ikilinganishwa na walimu wanaofunza shule za kijijini.

Tajiriba ya kufunza huboresha stadi ya kufundisha huku wanafunzi wakijifunza vyema zaidi mikononi mwa walimu ambao wamewafundisha kwa muda wa miaka mingi (Ijaiya, 2000). Schuler (1984) alipanga uzoefu wa ufunzaji katika makundi matatu (3-6, 7-10 na zaidi ya miaka 10). Matokeo yake yalionyesha kuwa malengo ya walimu walio na uzoefu wa juu zaidi yalikusisha zaidi somo kuliko ya wale walimu wanaofunza mwaka wao wa kwanza. Kwa mujibu wa Wall (2002) uzoefu wa kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho huathiri mitazamo ya walimu. Matokeo ya utafiti wake yalibaini kuwa, kuna uhusiano mkubwa kati ya maarifa aliyo nayo mwalimu kuhusu wanafunzi wenye ulemavu wa macho na mtazamo chanya kuhusu ujumuishaji wa wanafunzi hao. Rosenthal (2007) alitambua kuwa, shule nyingi zinazofaulu huwa na mchanganyiko mzuri wa walimu wenye tajiriba na walimu

wapya wasio na tajiriba. Anasisitiza kuwa, walimu walio na tajiriba huwashauri na kuwa kielelezo kizuri kwa walimu wapya ilhali walimu wapya huleta mawazo mapya na motisha ya kufanya kazi. Manufaa ya tajiriba huwa dhahiri baada ya miaka minne au mitano.

Athari hasi ilibainika wakati wa ujifunzaji wa stadi za kusoma na kuandika katika shule ya Menengai kwani kupitia uchunzaji na mahojiano na walimu ilitambulika kuwa, walimu wanne kati ya watano walikuwa na mtazamo hasi kuhusu ujumuishaji. Wengi wao walikiri kwamba wanafunzi wenye ulemavu wa macho waliwapotezea muda wanafunzi wasio na ulemavu wa macho, jambo lililowafanya kutowapa umakini unaowafaa ili waboreshe ustadi wao wa Kiswahili. Kinyume na shule ya Menengai walimu wanne kati ya watano waliohojiwa katika shule ya Joel Omino walikiri kuwa ujumuishaji wa wanafunzi walio na ulemavu wa macho ulikuwa na manufaa kwani walipata usaidizi kutoka kwa wanafunzi wenzao. Mtazamo huu chanya uliwasaidia walimu kuwashughulikia wanafunzi hawa ipasavyo katika shule hii. Ni wazi kuwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika shule ya Joel Omino wanajifunza stadi za lugha ya Kiswahili kwa ubora zaidi ikilinganishwa na shule ya Menengai kutokana na walimu wao kuwa na tajiriba ya juu zaidi ya kuwashughulikia.

4.5 Athari inayotokana na Mielekeo ya Watu

Bila shaka kuna tofauti ya kimtazamo kati ya mazingira ya mjini na mazingira ya kijijini. Wakazi wa mjini wana uelewa mzuri zaidi kuhusu ulemavu kuliko wakazi wa kijijini ambao mtazamo wao kuhusu ulemavu ni finyu kulingana na matokeo ya utafiti uliotekelezwa. Katika shule ya Joel Omino ilidhihirika kuwa hakukuwa na ushirikiano

kamilifu kati wa wazazi na walimu kwani baadhi ya wazazi wana mtazamo hasi kuhusu ulemavu kutokana na wao kukosa elimu. Iwapo baadhi ya wazazi hawa hawana uelewa huu, kuna uwezekano wao kukosa kununua vifaa vinavyohitajika katika ujifunzaji wa stadi za lugha. Ilithibitishwa kutokana na mahojiano na walimu na wanafunzi kuwa athari hasi katika ujifunzaji wa stadi za lugha ilitokana na kutokuwepo kwa ushirikiano kamilifu kati ya wazazi na walimu. Haya yalithibitishwa na mwalimu Ali aliyekiri kuwa;

Ushirikiano kati ya mwalimu na mzazi usipokuwa kamilifu, ujifunzaji huathirika kwani mzazi huhitajika kutoa habari muhimu kuhusu mtoto wake kama vile kiwango cha ulemavu alio nao. Habari hizi zisipotolewa ni vigumu mwalimu kujua jinsi anavyotakiwa kurekebisha ufunzaji wake kwani haelewi mahitaji ya mwanafunzi. Katika ujifunzaji wa stadi za lugha mikakati inafaa kuwekwa darasani ili mwanafunzi aliye na ulemavu wa macho aweze kupata mafunzo ya ubora. Mikakati hii ni kama vile, mahali ambapo anafaa kuketi darasani, vifaa vya ujifunzaji vinavyofaa kutumika na kadhalika. Katika ujifunzaji wa stadi ya kusoma na kuandika mwanafunzi aliye na ulemavu wa macho mara nyingi anafaa kuwekwa karibu na ubao lakini ikiwa mzazi hatashirikiana na mwalimu hivyo basi, athari hasi itaonekana katika matokeo.

Eneo la kijiografia la shule kulingana na Owoeye na Yara (2011) lina athari katika kufaulu kwa wanafunzi kitaaluma. Ayodele (1988) anasema kuwa, wanafunzi katika shule za msingi za mijini wanafaulu zaidi kuliko wanafunzi walio katika shule za vijijini katika lugha. Gardiner (2008) anaeleza kuwa hii inaweza kuwa ni kwa sababu ya ukosefu wa utamaduni wa kusoma katika jamii za vijijini, uchache wa vitabu, majarida au magazeti nyumbani, ukosefu wa maktaba na ukosefu wa umahiri wa lugha wa walimu katika shule za vijijini.

Kinyume na shule ya Joel Omino mtafiti alitambua kuwa katika shule ya Menengai kulikuwa na ushirikiano baina ya walimu na wazazi wa wanafunzi walio na ulemavu wa macho. Kutokana na kipengele hiki, kulikuwa na athari chanya katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili katika shule ya Menengai ikilinganishwa na shule ya Joel Omino. Kutokana na utafiti huu ilibainika kuwa wazazi wa mjini ni watu wenye mielekeo kubalifu kuhusu ulemavu ikilinganishwa na wazazi wa kijijini ambao wengi wao wana imani za kishirikina kuhusu ulemavu. Aidha, wanaharakati wengi ambao huendeleza mitazamo kuwa ulemavu si ukosefu wa uwezo wa kutenda mambo hupatikana mjini kuliko vijijini.

4.6 Athari ya Idadi ya Walimu na Wanafunzi

Mtafiti alitambua kutokana na mahojiano na uchunzaji kuwa vipengele vya mazingira ya darasani kama vile idadi kubwa ya wanafunzi madarasani na idadi ndogo ya walimu wa Kiswahili vilikuwa na athari hasi katika ujifunzaji wa stadi za lugha kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Idadi kubwa ya wanafunzi ilibainika katika shule mbili lengwa. Kulikuwa na wanafunzi takriban sabini katika kila darasa katika shule ya Menengai ilhali shule ya Joel Omino ilikuwa na wanafunzi takriban tisini katika kila darasa. Aidha, walimu waliohojiwa katika shule zote mbili walikiri kuwa idadi ya walimu wa Kiswahili ilikuwa ndogo ikilinganishwa na idadi kubwa ya wanafunzi katika kila darasa.

Mwalimu Aziza kutoka shule ya Menengai alikuwa na haya ya kusema kuhusu athari ya idadi kubwa ya wanafunzi madarasani;

Ujifunzaji wa stadi za lugha hutegemea mbinu tofauti za ufunzaji kama vile, kuwashirikisha wanafunzi katika majadiliano, wanafunzi kuigiza darasani, wanafunzi kusoma hadithi darasani kwa sauti na kadhalika. Kushiriki katika majadiliano darasani huwasaidia wanafunzi kukuza stadi ya kuandika na kuzungumza, kwani baada ya kujadiliana, wao huandika muhtasari wa mawazo na hoja mpya. Kwa upande mwingine, kuigiza darasani kunakuza stadi ya kuzungumza na kusikiliza kwa wanafunzi. Hata hivyo, kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi madarasani, mbinu hizi hazihusishwi sana katika somo hasa kutokana na mwalimu kupendelea kutumia mbinu ya kuhadhiri ili kuweza kufikia lengo lake ndani ya muda mchache na hili huwa na athari hasi katika ujifunzaji wa stadi za lugha.

Maelezo ya mwalimu Aziza yanalingana na maoni ya Nikolic (1987) anayedai kuwa, wanafunzi kufanya kazi katika vikundi hakufai kupuuzwa kwani ni muhimu katika ujifunzaji wa stadi ya kuandika. Anaendelea kusema kuwa, wanafunzi walio na ulemavu wa macho hufaidika katika kujifunza stadi ya kuandika na kusoma wanapofanya kazi katika vikundi kwani kiwango cha uwezo wa wanafunzi si sawa. Kwa hivyo, kazi inafaa kugawanywa kulingana na ugumu wake. Nabiryo na Sekiziyivu (2019) wanakubaliana na Nikolic (1987) kwa kusema kuwa, ujifunzaji wa stadi ya kuandika unahusisha mwingiliano wa mwanafunzi na mwalimu wao, wanafunzi wenzake na mazingira. Mwingiliano huu kulingana nao hufanyika wakati darasa lina utulivu, mwalimu ana ujuzi kuhusu somo na anawahimiza wanafunzi wake kujadili naye au wanafunzi wenzao kuhusu kazi ambayo wanaandika.

Aidha, Hinkel (2006) anashadidia maoni ya Nabiryo na Sekiziyivu (2019) anaposema kuwa, kuwashirikisha wanafunzi katika ujifunzaji wa stadi ya kuzungumza ya lugha ya

pili huwapa wanafunzi uwezo wa kuboresha ufasaha wao, usahihi na uchangamano wa lugha. Hata hivyo, Nikolic (1987) anasisitiza kuwa, kufanya kazi katika makundi huwa bora zaidi ikifanyika katika madarasa yaliyo na idadi ndogo ya wanafunzi, madai ambayo ni kinyume na hali iliyoko katika shule hizi mbili.

Katika shule ya Joel Omino idadi ya wanafunzi ilikuwa kubwa kupita kiasi ikilinganishwa na shule ya Menengai hata hivyo, athari zilikuwa zilezile zilizojitokeza katika shule ya Menengai. Walimu waliosailiwa walikubali kuwa wanafunzi walitazitika kujifunza stadi za lugha ya Kiswahili kutokana na idadi yao kubwa ikilinganishwa na idadi ya walimu wa Kiswahili wanaowafunza. Mwalimu Neema alisema kuwa;

Ili kujifunza stadi nne kuu za lugha kwa ufasaha kila mwanafunzi anafaa kushirikishwa katika mazoezi yatakayoboresha stadi hizi. Katika shule za msingi ili kukuza stadi ya kuandika wanafunzi wanahitajika kufanya kazi za ziada na kuandika insha. Hata kama kazi za ziada hupewa wanafunzi wote darasani bila kujali hali aliyo nayo mwanafunzi, mazoezi wanayopewa hayawatoshi kwani wakipewa kazi nyingi itakuwa mzigo kwa mwalimu kutokana na ukosefu wa muda wa kutosha. Aidha, katika uandishi wa insha mazoezi yanafaa kufanywa mara kwa mara ili wanafunzi wawe na ubora katika stadi hiyo. Hata hivyo, kutokana na idadi yao kubwa ni vigumu kufanya hivi. Suala hili hudumaza ujifunzaji wa stadi ya kuandika kwa kiasi kikubwa.

Maelezo ya Neema yanasadikishwa na Kuczynski (2012) anayeshikilia kuwa, wanafunzi wanapokuwa zaidi ya thelathini na wanne darasani itakuwa vigumu kuwafikia kibinafsi na kimaarifa mmoja baada ya mwingine wakati wa mchakato wa ufunzaji na ujifunzaji. Vilevile, Haq na wenzake (2020) wanasema kuwa, uandishi wa kazi ya ziada huboresha msamiati na mwendo wa uandishi wa mwanafunzi. Maoni ya

Kuczynski (2012) na Haq na wenzake (2020) yanashabihiana na yale ya Yelkpieri na wenzake (2012) ambao walibaini kuwa wanafunzi walio na udhaifu hawahudumiwi ifaavyo katika madarasa yaliyo na idadi kubwa ya wanafunzi. Hili linaonyesha kuwa uangalifu na umakini wa kibinafsi haupewi wanafunzi ambao wanaweza kuuhitaji zaidi. Kwa hivyo, wanafunzi ambao wanaweza kuwa na ugumu wa kuelewa somo wanapaswa kuona walimu na wanafunzi wenzao katika muda wao wa ziada au wanapaswa kufanya jitihada za ziada wao wenyewe ili kuelewa. Kwa mujibu wa wataalam hawa, hili haliendelezi ubora wa ufunzaji na ujifunzaji katika hali yoyote ile.

Kuhusu uchache wa walimu unavyoathiri ujifunzaji wa stadi za Kiswahili, mwalimu Nuru alidokeza kuwa;

Kutokana na walimu wa Kiswahili kuwa wachache, inawabidi washughulikie madarasa mengi ya Kiswahili kwa siku moja. Kando na kufunza madarasa mengi vilevile, wanawashughulikia wanafunzi wengi katika darasa moja. Hivyo basi, hakuna muda wa kutosha wa kutayarisha somo ipasavyo. Matumizi ya vifaa vya ujifunzaji ni muhimu katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili hata hivyo, ni vigumu kutayarisha vifaa hivi hasa vinavyotumiwa na wanafunzi walio na ulemavu wa macho.

Isitoshe, katika shule hizi lengwa kupitia uchunzaji ilishuhudiwa kuwa mbinu ambayo mwalimu alitumia katika kuwafundishia wanafunzi stadi ya kusoma ni kuwashirikisha wanafunzi wote katika kusoma kwa pamoja kwa wakati mmoja. Mwalimu alitumia mbinu hii kwa kuwa muda haukutosha wa kuwapa wanafunzi wote nafasi kutokana na idadi yao kuwa kubwa sana. Kutokana na mahojiano na walimu ilibainika kuwa mbinu hii si bora kwani kuna uwezekano wa wanafunzi kuachwa nyuma hasa wale wenye

ulemavu wa macho wanaohitaji muda zaidi ili waone maandishi yaliyo vitabuni kwani hawana vitabu vyao maalum.

Kinachodhihirika hapa kutokana na maoni ya walimu na uchunzaji ni kinyume na maoni ya Setti (2016) ambaye anasema kuwa, wanafunzi hupata matokeo bora katika kujifunza stadi ya kusoma katika madarasa yaliyo na idadi ndogo ya wanafunzi. Matokeo ya utafiti huu yalikuwa sawa na matokeo ya Setti (2016) ambaye alibaini kuwa, idadi kubwa ya wanafunzi haikuwaruhusu walimu kuwafikia wanafunzi wote. Kuwashirikisha katika shughuli ya kusoma, kuandika na kuzungumza kunaonekana kutowezekana kufanyika katika madarasa hayo kwa kuwa muda wa kufunza hauruhusu mwalimu kufuatilia kila mwanafunzi. Hata hivyo, kando na idadi ya wanafunzi madarasani katika shule hizi mbili jumishi kuwa kubwa, ilibainika kuwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule ya Joel Omino waliathirika zaidi katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili ikilinganishwa na wa shule ya Menengai kwani darasa moja katika shule hii lilikuwa na wanafunzi ambao wanafaa kujaza madarasa mawili.

4.7 Hitimisho

Mazingira ya ujifunzaji huwa na athari hasi au chanya katika ujifunzaji wa lugha. Iwapo mazingira ambamo ujifunzaji hufanyika si faafu kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho, ujifunzaji wao utatatizika. Athari za tofauti za kimazingira kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili zilizojitokeza katika uchunguzi huu ni; athari ya mazingira ya kelele, athari ya hali ya kiuchumi, athari ya usuli wa lugha, athari ya tajiriba ya kufunza, athari ya mielekeo ya

watu na athari ya idadi ya walimu na wanafunzi. Sura inayofuata imeshughulikia muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho la utafiti na mapendekezo ya tafiti za ziada.

SURA YA TANO

MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

5.0 Utangulizi

Tasnifu hii ilikusudia kulinganisha ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule mbili jumuishi, moja ikiwa katika mazingira ya mjini yanayosheheni wingi lugha na nyingine katika kitongoji cha mji ambao wakazi wake kwa kiasi kikubwa huzungumza lugha moja. Sura hii, imeshughulikia muhtasari wa tasnifu hii. Vilevile, imeshughulikia muhtasari wa matokeo ya utafiti kuhusu ulinganishaji wa ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi katika Kaunti za Nakuru na Kisumu. Tutahitimisha sura hii kwa kutoa mapendekezo yanayotokana na utafiti na pia kutoa mapendekezo yanayostahili kushughulikiwa na tafiti za baadaye.

5.1 Muhtasari wa Utafiti

Sura ya kwanza ilihusu utangulizi ambapo ilibainisha suala la utafiti, malengo na maswali yaliyoongoza utafiti huu. Katika kutoa sababu za kuchagua mada, mtafiti alieleza mantiki ya kufanya utafiti huu. Tafiti za awali ambazo zilichangia kuboresha utafiti huu, mbinu za utafiti, nadharia na pia hoja zilizotumika zilizadiliwa.

Sura ya pili imeshughulikia tofauti za changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi za msingi za Menengai na Joel Omino katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili. Changamoto zilizojitokeza katika shule ya Menengai na Joel Omino ziligawanywa katika matapo matatu yaani; changamoto

zinazotokana na mazingira ya darasani, nyumbani na shuleni. Changamoto nyingi ziliwiana katika shule lengwa. Hata hivyo, kuna tofauti katika hoja ya ushirikiano kutoka kwa wazazi na maeneo ambapo shule inapatikana.

Sura ya tatu imeshughulikia tofauti za usuli wa mazingira ya ujifunzaji kati ya shule jumuishi ya Menengai na Joel Omino. Aidha, mtafiti amelinganisha usuli wa mazingira kati ya shule jumuishi ya msingi ya Menengai ambayo inapatikana mjini ambapo kwa kawaida, kuna wingi lugha na shule jumuishi ya msingi ya Joel Omino ambayo asilimia kubwa ya wanafunzi katika shule hii inazungumza lugha moja ya kwanza. Mtafiti alitambua tofauti tano za kimazingira kati ya shule mbili zilizolengwa katika uchunguzi huu.

Sura ya nne imeshughulikia athari za tofauti za kimazingira kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa stadi za Kiswahili. Mtafiti alieleza jinsi tofauti ya mazingira ya shule jumuishi zilizoko mjini na kijijini huathiri ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili. Kutokana na uchanganuzi wa data mtafiti alibaini athari za mazingira kufanana na kutofautiana katika shule mbili lengwa.

5.2 Matokeo ya Utafiti

Kutokana na uchanganuzi wa data, mtafiti alitambua matokeo yafuatayo ambayo yameelezwa moja baada ya nyingine. Katika sura ya pili, mtafiti alibainisha tofauti za changamoto zinazowakumba wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi ya Menengai na Joel Omino katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Changamoto ambazo mtafiti alibaini kutokana na uchanganuzi wa data zilizigawa

katika matapo matatu; changamoto zinazotokana na mazingira ya darasani ambazo ni; muda wa ufunzaji na ujifunzaji, ukosefu wa ujuzi wa walimu, idadi kubwa ya wanafunzi madarasani, mtazamo hasi wa wanafunzi na walimu, ukosefu wa vitabu vifaavyo na vifaa vya ufunzaji na ujifunzaji, idadi ndogo ya walimu wanaofunza somo la Kiswahili, kutegemea wanafunzi wasio na ulemavu wa macho. Changamoto zinazotokana na mazingira ya nyumbani; ushirikiano kutoka kwa wazazi, hali ya umaskini na vilevile, changamoto zinazotokana na mazingira ya shuleni; maeneo ambapo shule inapatikana. Kati ya changamoto kumi zilizotambulika ilibainika kuwa, changamoto mbili ambazo ni ushirikiano kutoka kwa wazazi na maeneo ambapo shule inapatikana zilitofautiana katika shule mbili lengwa.

Katika sura ya tatu, mtafiti alitambua kutokana na utafiti kuwa tofauti hizi ni kama vile; tofauti ya walimu wa kiswahili kati ya shule mbili lengwa, tofauti ya ushirikiano wa wazazi kati ya shule ya Menengai na Joel Omino, tofauti ya tajiriba ya walimu kati ya shule jumuishi lengwa, tofauti ya upatikanaji wa chumba maalum katika shule lengwa na tofauti ya usuli wa lugha kati ya shule ya Menengai na Joel Omino. Mtafiti alibaini kuwa, shule ya Menengai ilikuwa na mwalimu mmoja mwenye ulemavu wa macho, yaani upofu kamili. Tofauti na shule ya Menengai, shule ya Joel Omino haikuwa na mwalimu wa aina hiyo. Aidha, mtafiti alithibitisha kuwa katika shule jumuishi ya Joel Omino ushirikiano wa wazazi na shule ulikuwa wa kiwango cha chini ikilinganishwa na shule jumuishi ya msingi ya Menengai. Vilevile, katika shule ya Menengai, ilidhihirika kuwa, walimu wote waliowashughulikia wanafunzi walio na ulemavu wa macho walikuwa na tajiriba ya chini ya miaka mitano. Hali ilikuwa tofauti katika shule ya Joel

Omino ambapo walimu wawili walikuwa na tajiriba ya zaidi ya miaka kumi, mmoja akiwa na tajiriba ya zaidi ya miaka mitano na hatimaye, mwalimu mmoja akiwa na tajiriba ya miezi minne.

Tofauti nyingine ya kimazingira iliyojitokeza katika shule lengwa ilikuwa ni upatikanaji wa chumba maalum. Katika shule ya Menengai kulikuwa na chumba maalum ambacho kilitumiwa na wanafunzi wenye ulemavu wa macho. Kinyume na shule ya Menengai, matokeo ya uchunzaji na mahojiano na walimu na wanafunzi walio na ulemavu wa macho, katika shule ya Joel Omino yalidhihirisha kuwa hakukuwa na chumba maalum. Isitoshe, shule ya Menengai na Joel Omino zina tofauti ya usuli wa lugha kutokana na mazingira yao tofauti. Ilidhihirika kuwa, Kaunti ya Nakuru ni mazingira ya wingi lugha ambapo wakazi wake wanatumia lugha mseto ilhali mazingira ya usuli wa lugha katika shule ya Joel Omino yalikuwa tofauti kwani lugha asili zinazozungumzwa na wanafunzi zaidi ni Dholuo, Ekegusii na Kiluhya.

Katika sura ya nne, mtafiti alichambua athari za tofauti za kimazingira kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili katika shule lengwa. Matokeo ya utafiti yalithibitisha athari sita; athari ya mazingira ya kelele, athari inayotokana na hali ya kiuchumi, athari ya usuli wa lugha, athari ya tajiriba ya kufunza, athari inayotokana na mielekeo ya watu, athari ya idadi ya walimu na wanafunzi. Kutokana na matokeo haya, ni dhahiri kuwa mazingira tofauti ya shule hizi mbili jumuishi yana athari hasi na chanya katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili.

5.3 Mapendekezo Kutokana na Utafiti

Mapendekezo yanayowasilishwa hapa yanatokana na matokeo ya utafiti huu na yanalenga kuchangia katika kuimarisha ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi. Mapendekezo hayo ni; Kutokana na kuwa baadhi ya walimu hawana tajiriba ya kufunza wala maarifa ya sera ya ujumuishaji, serikali inafaa kutoa mafunzo ya kutosha kabla ya kuanza kufunza na kuendelea wanapohudumu katika kazi zao ili waweze kuwapa mafunzo yanayostahili wanafunzi wenye ulemavu wa macho yatakayowawezesha kuboresha ujifunzaji wao wa stadi za lugha.

Ili kuhakikisha wazazi wanaimarisha mazingira ya nyumbani ambayo yatawafaa wanafunzi wao katika somo la Kiswahili na masomo mengine kwa jumla, serikali ya kitaifa inapaswa kuhakikisha kuwa wazazi wanapewa mafunzo kuhusu umuhimu wa elimu ya wanafunzi wenye ulemavu na hasa wenye ulemavu wa macho na jinsi ya kuwashughulikia. Aidha, wazazi, walimu, wanafunzi na wataalam wa elimu jumuishi waungane mkono ili waunde mazingira mazuri ya ujumuishaji yatakayopunguza vizuizi vinavyowakabili wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika mchakato wao wa ujifunzaji. Utafiti huu umeonyesha walimu wengi hawana tajiriba au mafunzo ya kushughulikia wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi, hivyo basi, serikali inafaa kuwaajiri walimu zaidi walio na mafunzo ya kuwashughulikia wanafunzi wenye ulemavu ili waweze kuwashughulikia wanafunzi hao katika madarasa jumuishi.

Aidha, kutokana na hali maalum ya shule jumuishi, kuna haja ya serikali kuajiri wasaidizi wa darasani ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika madarasa jumuishi hawaachwi nyuma. Hili litampunguzia mwalimu mzigo ili aweze kufunza darasa nzima, na pia kuhakikisha wanafunzi wanaoona hawatumii muda wao kuwashughulikia wenzao wenye ulemavu wa macho. Isitoshe, kutokana na kuwa idadi ya wanafunzi katika shule mbili lengwa ni kubwa kupita kiasi, idadi ya wanafunzi madarasani inafaa kupunguzwa ili kufanikisha ujifunzaji wa stadi za lugha kwa ufasaha na wanafunzi walio na ulemavu wa macho kupata nafasi ya kutangamana na mwalimu ili kujihisi kuwa katika sehemu ya mchakato wa ujifunzaji wa stadi hizi.

Vilevile, utafiti huu unapendekeza shule zishirikiane na mashirika yasiyo ya kiserikali ili kuboresha uchapishaji wa vitabu vilivyo na sauti, vitabu vya breli na vilevile vitabu vilivyo katika maandishi makubwa. Vitabu vifaavyo na vifaa vya ujifunzaji vinafaa kupatikana ili kiwango cha wanafunzi wenye ulemavu wa macho kuwategemea wasio na ulemavu wa macho kipunguzwe katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili. Isitoshe, ni muhimu kuboresha vifaa hivyo ili vishughulikie mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho.

5.4 Mapendekezo Kuhusu Tafiti za Baadaye

Utafiti huu ulilenga kulinganisha ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi katika Kaunti za Nakuru na Kisumu. Kutokana na suala hili kutofanyiwa utafiti mwingi nchini Kenya, tafiti zaidi zifuatazo zinaweza kufanywa: Kwanza, kwa vile utafiti huu ulifanywa kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho katika darasa la nne hadi la saba katika Kaunti ya Nakuru

na Kisumu, pana haja ya utafiti mwingine kufanywa katika Kaunti zingine nchini na pia katika kiwango cha shule jumuishi za upili. Vilevile, utafiti mwingine ufanywe kuhusu ujifunzaji wa vipengele vingine vya lugha kama vile, uandishi wa insha, msamiati na vipengele vinginevyo vya Kiswahili kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi.

Aidha, kuna haja ya utafiti kufanywa kuhusu ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi au maalum kwa kutumia nadharia nyinginezo ili kuzalisha maarifa zaidi. Isitoshe, utafiti wa aina hii unafaa kufanywa kwa wanafunzi wenye ulemavu wa aina nyingine katika shule jumuishi na vilevile, katika shule maalum. Mwisho, kuwe na utafiti wa ulinganishaji wa ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi na pia shule maalum.

Marejeleo

- Achayo, E. (2003). *A Morphosyntactic of Dholuo Verbs Using Minimalist Program Approach* (Unpublished Masters Thesis). Nairobi University.
- Adetoro, N. (2012). Alternative Format Preferences Among Secondary School Visually Impaired Students in Nigeria. *Journal of Librarianship and Information Science*, 44(2), 90-96.
- Adicka, P. O. (2016). *Utohozi wa Maneno-mkopo katika Lugha ya Kijaluo kutoka Kiswahili: Mtazamo wa Mlingano Chanzi* (Tasnifu ya Uzamili, Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Agesa, L. (2014). Challenges Faced by Learners with Visual Impairments in Inclusive Setting in Trans-Nzoia County. *Journal of Education and Practice*, 5(29), 185-192.
- Al-Zoubii, S. M., & Rahmani, M. S. B. A. (2012). The Effect of Resource Room on Improving Reading and Arithmetic Skills for Learners with Learning Disabilities. *The International Journal of Scientific Research in Education*, 5(4), 269-277.
- Arslantas, T. K. (2017). Foreign Language Education of Visually Impaired Individuals: A Review of Pervasive Studies. *IHEAD: Ihlara Journal of Educational Research*, 2(2), 95-104.
- Atkinson, D. (1993). *Teaching Monolingual Classes* (Vol. 12). London: Longman.
- Aydoğan, H., & Akbarov, A. A. (2014). The Four Basic Language Skills, Whole Language & Intergrated Skill Approach in Mainstream University Classrooms in Turkey. *Mediterranean Journal of Social Sciences*, 5(9), 672-672.
- Ayodele, S.O (1988). A Study of the Relative Effects of the Problems of Class Sizes and Location of Schools on Performance of Pupils. In *Nigerian Journal of Curriculum Studies*, Vol. VI, No.2.
- Bamba, M. (2012). *Seeking Effective Approaches to Teaching Large EFL Classes in the Ivory Coast* (Published Doctoral Dissertation). Indiana University of Pennsylvania.
- Barron, A. E. (2004). Auditory Instruction. In D. H. Jonassen (Ed.), *Handbook of research in educational communications and technology* (pp. 949-978). Mahwah, NJ: Erlbaum

- Başaran, S. (2012). Teaching English to Visually Impaired Students in Turkey: A case study. *Energy, Education, Science and Technology Part B: Social and Educational Studies*, 2, 217-226.
- Beardsmore, H. B. (1982). *Bilingualism: Basic Principles*. Clevedon, Uk: Multilingual Matters.
- Bhela, B. (1999). Native Language Interference in Learning a Second Language: Exploratory Case Studies of Native Language Interference with Target Language Usage. *International Education journal Vol 1, No 1, 1999*.
- Bruner, J. S. (1966). *Toward a Theory of Instruction* (Vol. 59). Harvard University.
- Bukoye, R. O. (2019). Utilization of Instruction Materials as Tools for Effective Academic Performance of Students: Implications for Counselling. In *Multidisciplinary Digital Publishing Institute Proceedings* (Vol. 2, No. 21, p. 1395).
- Carasco, J. (1996). Universal Primary Education Registration Monitoring Report. *Kampala Ministry of Education and Sports*.
- Careless, D. (2008). Student Use of the Mother Tongue in the Task-Based Classroom. *ELT Journal, Volume 62, No. 4, 331- 337*.
- Cook, C. R., Grady, E. A., Long, A. C., Renshaw, T., Coddling, R. S., Fiat, A., & Larson, M. (2017). Evaluating the Impact of Increasing General Education Teachers' Ratio of Positive to Negative Interactions on Students' Classroom Behavior. *Journal of Positive Behavior Interventions*, 19(2), 67-77.
- Dechert, H. W. (1983). *How a Story is Done in a Second Language in Strategies in Interlanguage Communication*, Eds. C. Faerch And G. Kasper, Longman, London.
- Delgado-Gaitan, C. (1991). Involving Parents in the Schools: A Process of Empowerment. *American Journal of Education*, 100(1), 20-46.
- Duhaney, D. C., & Duhaney, L. M. G. (2000). Assistive technology: Meeting the Needs of Learners with Disabilities. *International Journal of Instructional Media*, 27, 393-401.
- Ellis, R. (1997). *Second Language Acquisition*. Oxford University Press, Oxford.
- Gardiner, M. (2008). *Education in rural areas*. Issues in education policy, 4, 1-33.

- Gass, S. M., & Selinker, L. (2001). *Second Language Acquisition: An Introductory Course*. Mahwah, NJ: Lawrence Erlbaum Associates.
- Githinji, P. (2006). Bazes and their Shibboleths: Lexical Variation and Sheng Speakers' Identity in Nairobi. *Nordic Journal of African Studies*, 15(4), 443-472.
- Gompel, M., Vanbon, W. H. J. & Schreuder, R. (2004) Reading by Children with Low Vision. *Journal of Visual Impairment and Blindness* 98(2): 77–89.
- Hannum, E., & Zhang, Y. (2012). Poverty and Proximate Barriers to Learning: Vision Deficiencies, Vision Correction and Educational Outcomes in Rural Northwest China. *World Development*, 40(9), 1921-1931.
- Haq, M. N. U., Mahmood, M., & Awan, K. (2020). Assistance of Formative Assessment in the Improvement of English Writing Skills at Intermediate Level. *Global Language Review*. V(III), 34-41.
- Harris, K. R., & Graham, S. (1996). Constructivism and Students with Special Needs: Issues in the Classroom. *Learning Disabilities Research and Practice*, 11, 134-137.
- Haugann, E. M. (1987). Visually Impaired Students in Higher Education in Norway. *Journal of Visual Impairment and Blindness*, 81(10), 482-484.
- Hauk, A. (2009). *No Teacher Left Behind: The Influence of Teachers with Disabilities in the K-8 Classrooms. A Review of the Literature* (Unpublished Doctoral dissertation). University of Alaska Southeast.
- Heward, W. L.(2000). *Exceptional Children: An Introduction to Special Education*. Upper Saddle River, New Jersey. Prentice-Hall.
- Hinkel, E. (2006). Current perspectives on teaching the four skills. *Tesol Quarterly*, 40(1), 109-131.
- Hornby, G. (1995). *Working with Parents of Children with Special Needs*. London: Cassell.
- Ijaiya, N. Y. (2000). Failing Schools' and National Development: Time for Reappraisal of School Effectiveness in Nigeria. *Niger. J. Educ. Res. Eval.*(2), 2, 42.
- Jobe, D., Rust, J. O., & Brissie, J. (1996). Teacher Attitudes Toward Inclusion of Students with Disabilities into Regular Classrooms. *Education*, 117(1), 148-154.

- Kapur, R. (2018). "Challenges Experienced by Visually Impaired Students in Education." https://www.researchgate.net/publication/323833804_Challenges_Experienced_by_Visually_Impaired_Students_in_Education (Accessed 14 September 2019).
- Karim, K., & Nassaji, H. (2013). First Language Transfer in Second Language Writing: An Examination of Current Research. *Iranian Journal of Language Teaching Research*, 1(1), 117-134.
- Keefe, J. (1994). Assessment of Low Vision in Developing Countries—World Health Organization Programme for Prevention of Blindness. *University of Melbourne, Australia*.
- Kiatkheeree, P. (2018). Learning Environment for Second Language Acquisition: Through the Eyes of English Teachers in Thailand. *International Journal of Information and Education Technology*, 8(5), 391-395.
- Kuczynski-Brown, A. (2012). New York Class Size: Nearly Half of Public Schools Have Overcrowded Classrooms, UFT Says. *Huffington Post*.
- Kurniasih, E. (2011). Teaching the Four Language Skills in Primary EFL Classroom. *JET (Journal of English Teaching)*, 1(1), 70-81.
- Kuyini, A. B., & Desai, I. (2007). Principals' and Teachers' Attitudes and Knowledge of Inclusive Education as Predictors of Effective Teaching Practices in Ghana. *Journal of Research in Special Educational Needs*, 7(2), 104-113.
- Lado, R. (1960). *Linguistics Across Culture*. Ann Arbor, MI: The University of Michigan Press.
- Lamichhane, K. (2017). Teaching Students with Visual Impairments in an Inclusive Educational Setting: A Case from Nepal. *International Journal of Inclusive Education*, 21(1), 1-13.
- Lane, C. M. (2008). *Predictors of successful inclusion for children with vision impairment in early education* (Unpublished Doctoral dissertation). Curtin University.
- Learning, S. (2003). Teaching Students with Visual Impairment: A Guide for the Support Team. *Regina, Saskatchewan, Canada*.
- Lewis, R. B., Wheeler, J. J., & Carter, S. L. (2017). *Teaching Students with Special Needs in General Education Classrooms*. New Jersey: Pearson Education.

- Lewis, S., Corn, A. L., Erin, J. N., & Holbrook, M. C. (2003). Strategies Used by Visually Impaired Teachers of Students with Visual Impairments to Manage the Visual Demands of Their Professional Role. *Journal of Visual Impairment & Blindness*, 97(3), 157-168.
- Lichuma, S. K. (2018). *Mikakati ya Kufundishia Stadi ya Kusoma kwa Kutumia Vitabu vya Hadithi, katika Shule za Msingi za Kaunti ya Kakamega Nchini Kenya* (Tasnifu ya Uzamili, Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Masinde Muliro.
- Lodhi, M. A., Sahar, A. H., Qayyum, N., Iqbal, S., & Shareef, H. (2019). Relationship of School Environment and English Language Learning at Government Schools. *Public Administration Research*, 8(1), 1-13.
- Maemba, L. S., Maina, A., & Ogola, F. O. (2016). Primary Schools' Preparedness to Integrate Visually Impaired Learners Into Inclusive Education in Bomet County, Kenya. *International Journal of Innovative Research and Advanced Studies*, 3(8), 1-10.
- Manrique, C. M. R. (2013). Mother Tongue Interference Over Foreign Language: A Case Study About A2 Oral Production in a Colombian Public University. *Opening Writing Doors Journal*, 9(1), 91-119.
- Marfo, R., Mensah, J. K., & Nantwi, W. K. (2020). Making Inclusive Education a Reality: The Role of Teachers, Parents and Administrators. *European Journal of Education Studies*, 7(2), 1-29.
- Mekonge, L. N. (2016). *Athari za Sheng' katika Ufundishaji wa Kiswahili Mjini Kisii: Utafiti Kifani wa Shule za Upili za Gusii Highlights na Daraja Mbili* (Unpublished Doctoral Dissertation). University of Nairobi.
- Melly, K. J. (2019). *Matumizi ya Vifaa vya Kisasa katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Sarufi: Mfano wa Shule za Upili za Kaunti Ndogo ya Moiben, Kenya* (Tasnifu ya Uzamili, Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kibabii.
- Momanyi, C. (2009). The Effects of 'Sheng' in the Teaching of Kiswahili in Kenyan Schools. *Journal of Pan African Studies*, vol.2, no.8.
- Mwakyeja, B. M. (2013). *Teaching Students with Visual Impairments in Inclusive Classrooms, A Case Study of One Secondary School in Tanzania* (Unpublished Masters Thesis). University of Oslo.
- Nabiryo, N. R., & Sekiziyivu, S. (2019). The Influence of Classroom Environments on English Language Writing Instruction and Learning. *Journal of Language Teaching and Research*, 10(1), 68.

- Nikolic, T. (1987). Teaching a Foreign Language in Schools for Blind and Visually Impaired Children. *Journal of Visual Impairment & Blindness*, 81(2), 62-66.
- Njoroge, S. N. (2019). Effects of Teaching and Learning Resources in Lower Primary School Children in the Eastern Zone of Nakuru Municipality, Kenya. *Saudi Journal of Humanities and Social Sciences*, 4(12), 776-782.
- Nolan, C. Y., & Morris, J. E. (1973). *Aural Study Systems for the Visually Handicapped*. Final Report. Kentucky, American Printing House for the Blind, Inc.
- Noor, H. H. (1994). Some Implications of the Role of the Mother Tongue in Second Language Acquisition. *Linguistica Communicatio*, 6, 97-106.
- O'brien, R. (1973). The Integrated Resource Room for Visually Impaired Children. *Journal of Visual Impairment & Blindness*, 67(8), 363-368.
- Odlin, T. (1989). *Language Transfer: Cross-Linguistic Influence in Language Learning*. Cambridge University Press.
- Oduor, C., Inyani, K. S., & Kobia, M. J. (2013). Athari za Uhamishaji wa Sarufi ya Kiluo kwenye Upatanisho wa Sarufi ya Kiswahili. *Kiswahili*, 76(1).
- Otyola, W. R., Kibanja, G. M., & Mugagga, A. M. (2017). Challenges Faced by Visually Impaired Students at Makerere and Kyambogo Universities. *Makerere Journal of Higher Education*, 9(1), 75-86.
- Owoeye, J. S., & Yara, P. O. (2011). School Location and Academic Achievement of Secondary School in Ekiti State, Nigeria. *Asian Social Science*, 7(5), 170-175.
- Parshall, C. G. (1999). Audio CBTs: Measuring More through the Use of Speech and Non-Speech Sound. Paper presented at the Annual meeting of the American Educational Research Association, Montreal, Canada, April 19-23.
- Pathan, M., Aldersi, Z., & Alsout, E. (2014). Speaking in their Language: An Overview of Major Difficulties Faced by the Libyan EFL Learners in Speaking Skill. *International Journal of English Language & Translation Studies*, 2(3), 96-105.
- Rosenthal, L. (2007). "Teacher experience and credentials: Issues to consider." *Great Schools*. Apr, 13.
- Rost, M. (2002) *Teaching and Researching Listening*. London: Longman.

- Schuler, G. W. (1984). *The Effect of Teaching Experience on Teachers' Perceptions of their Teacher-Preparation Programs* (Unpublished Doctoral Dissertation). Temple University.
- Schunk, D. H. (2008). *Learning Theories* (5th ed.). Upper Saddle River, NJ: Pearson Education, Inc.
- Seligman, M. (2000). *Conducting Effective Conferences with Parents of Children with Disabilities: A Guide for Teachers*. New York: Guilford Press.
- Setti, F. (2016). *The Problem of Overcrowded Classes in Learning English as a Foreign Language Case Study: First Year LMD Students of English at Mohamed Kheider* (Unpublished Doctoral Dissertation). University of Biskra.
- Sherpa, D., & Baraily, K. (2021). Exploration of Teachers' Role in Resource Class: A Case from an Integrated School. *AMC Journal*, 2(1), 41-55.
- Shield, B., & Dockrell, J. (2008). The Effects of Classroom and Environmental Noise on Children's Academic Performance. In *9th International Congress on Noise as a Public Health Problem (ICBEN)*, Foxwoods, CT.
- Shrestha, S. (2017). Breaking the Barriers: The Journey of Students with Disabilities to Higher Education. *The Journal of University Grants Commission*, 6(1), 141-151.
- Sikanku, S. T. (2018). Challenges in Teaching Pupils with Visual Impairment in Inclusive Classrooms: The experience of Ghanaian teachers. *Journal of research on humanities and social sciences*, 8(11).
- Simon, C., Echeita, G., Sandoval, M., & Lopez, M. (2010). The Inclusive Educational Process of Students with Visual Impairments in Spain: An Analysis from the Perspective of Organizations. *Journal of Visual Impairment & Blindness*, 104(9), 565-570.
- Storey, K. (2007). Combating Ableism in Schools. *Preventing School Failure: Alternative Education for Children and Youth*, 52(1), 56-58.
- Subandowo, D. (2017). The Language Interference in English Speaking Ability for EFL Learners. *Proceedings of ISELT FBS Universitas Negeri Padang*, 5, 205-210.
- Susanto, S., & Nanda, D. S. (2018). Teaching and Learning English for Visually Impaired Students: An Ethnographic Case Study. *English Review: Journal of English Education*, 7(1), 83-92.

- Vikoo, B (2003). *Learning Theories and Instructional Process*, Owerri: Springfield Publishers Ltd.
- Wall, R. (2002). Teachers' Exposure to People with Visual Impairments and the Effect on Attitudes Toward Inclusion. *RE: view*, 34(3), 111-119.
- Webster, A., & Roe, J. (1998). *Children with visual impairments: Social interaction, language and learning*. Psychology Press.
- Williams, B., Williams, J., & Ullman, A. (2002). *Parental Involvement in Education*. London: Queens Printer.
- Yelkpieri, D., Namale, M., Esia-Donkoh, K., & Ofosu-Dwamena, E. (2012). Effects of Large Class Size on Effective Teaching and Learning at the Winneba Campus of the UEW (University Of Education, Winneba), Ghana. *Online Submission*.

VIAMBATISHO

Kiambatisho A: Maswali ya Mahojiano kwa Walimu wa Kiswahili

1. Umefundisha katika shule hii kwa muda upi?
2. Unafundisha somo la Kiswahili katika darasa lipi?
3. Umefundisha darasa hilo au madarasa hayo kwa miaka mingapi?
 - Tajiriba yako imekusaidiaje katika kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho?
4. Katika chuo cha ualimu au chuo kikuu, ulitayarishwa kuwahudumia wanafunzi walio na mahitaji maalum?
5. Ni changamoto zipi unazipata katika kuwafundisha wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule hii ili kuwasaidia kuimarisha ustadi wao wa Kiswahili?
 - Athari ni zipi zinazotokana na changamoto ulizozitaja katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi walio na ulemavu wa macho?
6. Je, wewe hutumia mbinu gani kufundishia unapofunza stadi za lugha ya Kiswahili ulizopewa ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu wa macho?
 - Kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika.
7. Je, unawapa wanafunzi walio na ulemavu wa macho mazoezi ya ziada ikilinganishwa na wale wasio na ulemavu wa macho ili kuboresha ujifunzaji wao wa Kiswahili? (ndiyo au la?)
 - Kama ndiyo, unawapa mazoezi ya aina gani wanafunzi walio na ulemavu wa macho?
8. Mazingira ya darasani katika shule hii yanawafaa wanafunzi wenye ulemavu wa macho? (ndiyo au la?)
 - Eleza kwa nini.
9. Ni mikakati ipi inayotekelezwa humu shuleni ambayo huathiri ujifunzaji wa Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho?
10. Kuweko kwa shule hii katika mazingira ya mjini au kijijini kuna athari zipi katika ufundaji na ujifunzaji wa Kiswahili.

11. Una maoni mengine yoyote ambayo ungependa kutoa kuhusu sera ya elimu jumuishi hasa katika ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili?

Kiambatisho B: Maswali ya Mahojiano kwa Wanafunzi Walio na Ulemavu wa

Macho

1. Ni changamoto zipi unazozipitia unaposoma somo la Kiswahili pamoja na wanafunzi ambao hawana matatizo ya kuona?
2. Katika somo la Kiswahili, wewe hufanya vizuri zaidi katika kuzungumza, kusikiliza, kusoma au kuandika?
 - Je, unafikiri ni sababu zipi zinakufanya ufanye vizuri katika stadi uliyosema kuwa una ustadi mzuri ikilinganishwa na stadi hizi zingine?
3. Changamoto zako huwa zipi katika kila stadi uliyopewa?
 - a) Kusoma.
 - b) Kuandika.
 - c) Kuzungumza.
 - d) Kusikiliza.
4. Eleza mambo yote ambayo yanakusaidia katika kujifunza Kiswahili ukiwa huku shuleni.
5. Je, unashirikiana na wanafunzi wenzako wasio na ulemavu wa macho katika ujifunzaji wa Kiswahili?
6. Ni mambo yepi ya nyumbani ambayo yanakusaidia katika kujifunza Kiswahili.
7. Ni mambo yepi ya nyumbani ambayo hukuzuia kujifunza Kiswahili vizuri?
8. Eneo ambalo shule yako inapatikana hukusaidia au hukuzuia kujifunza Kiswahili?
9. Unapendelea kuwa katika shule hii au ungependelea kuwa katika shule maalum ya watu wenye matatizo ya kuona?

**Kiambatisho C: Maswali ya Hojaji kwa Wanafunzi Walio na Wasio na Ulemavu
wa Macho**

Mimi ni Abunga Lilian Muguche, mwanafunzi wa shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nimetayarisha hojaji hii kutafiti kuhusu ulinganishaji wa ujifunzaji wa stadi za lugha ya Kiswahili kwa wanafunzi wenye ulemavu wa macho katika shule jumuishi katika Kaunti za Nakuru na Kisumu, Kenya. Nakuomba utenge muda wa kujibu maswali ya hojaji hii. Ninaahidi ya kwamba habari zote utakazotoa zitahifadhiwa kwa siri wakati na baada ya utafiti huu.

Maagizo;

Nakuomba uweke kikwaju katika visanduku ulivyopewa. Pale ambapo unahitajika kufafanua jibu lako, nakuomba utenge muda wa kueleza jibu lako kwa kina.

1. Jinsia yako?

Kiume	
Kike	

2. Una umri gani? Miaka _____

3. Nyumbani ni mtaa gani? Mtaa wa _____

4. Unasoma darasa lipi? Darasa la _____

5. Wazazi wako nyumbani wana ulemavu wa macho ?

Ndiyo	
La	

6. Je, nyumbani kuna mtu ambaye ana ulemavu wa aina nyingine?

- Ikiwa ndiyo, taja aina ya ulemavu _____

7. Unazungumza lugha ulizopewa kwa kiasi gani?

- a) Kiswahili -----%
- b) Kiingereza -----%
- c) Nyingine (Iandike) -----%
- d) Nyingine (Iandike) -----%

8. Panga stadi za lugha ya Kiswahili ulizopewa ukianza na ile ambayo unafanya vizuri zaidi na kumalizia na ile ambayo hufanyi vizuri sana kwa kutumia nambari ya kwanza ikiwa ile ambayo unafanya vizuri zaidi, ya nne ikiwa ile ambayo hufanyi vizuri zaidi.

- Kusoma _____
- Kuandika _____
- Kuzungumza _____
- Kusikiliza _____

9. Je, wewe hushirikiana na wanafunzi wenzako katika ujifunzaji wa

Kiswahili?

Ndiyo	
La	

10. Ikiwa una shida ya macho, unashirikiana na wenzako ambao hawana shida ya

macho katika kujifunza Kiswahili?

Ndiyo	
La	

11. Ikiwa wewe huna shida ya kuona, unashirikiana na wenzako katika kujifunza Kiswahili?

Ndiyo	
La	

12. Je, wewe hushirikiana na wenzako wenye shida ya kuona/wasio na shida ya kuona kwa hiari au kwa sababu mwalimu amekuomba kushirikiana?

Kiambatisho D: Vibali vya Kufanya Utafiti



KENYATTA UNIVERSITY GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke

Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100

NAIROBI, KENYA

Tel. 8710901 Ext. 57530

Our Ref: C50/NKU/CE/34302/2017

DATE: 22nd July, 2021

Director General,
National Commission for Science, Technology
and Innovation
P.O. Box 30623-00100
NAIROBI

Dear Sir/Madam,


RE: RESEARCH AUTHORIZATION FOR ABUNGA LILIAN MUGUCHE – REG. NO. C50/NKU/CE/34302/2017.

I write to introduce **Abunga Lilian Muguche** who is a Postgraduate Student of this University. The student is registered for M.A degree programme in the **Department of Kiswahili**.

Abunga intends to conduct research for a M.A Project Proposal entitled, “**Ulinganishaji wa Ujifunzaji Stadi za Kiswahili kwa Wanafunzi wenye Ulemavu wa macho katika Shule Jumuishi katika Kaunti za Nakuru na Kisumu, Kenya**”.

Any assistance given will be highly appreciated.

Yours faithfully,



PROF. ELISHIBA KIMANI
AG. DEAN, GRADUATE SCHOOL



AM/nn



**KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL**

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke

Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 810901 Ext. 4150

Internal Memo

FROM: Dean, Graduate School

DATE: 22nd July, 2021

TO: Abunga Lilian Muguche
C/o Kiswahili Dept.

REF: C50/NKU/CE/34302/2017

SUBJECT: APPROVAL OF RESEARCH PROPOSAL

We acknowledge receipt of your revised Research Proposal as per our recommendations raised by the Graduate School Board of 25th June, 2021 entitled “**Ulinganishaji wa Ujifunzaji Stadi za Kiswahili kwa Wanafunzi wenye Ulemavu wa macho katika Shule Jumuishi katika Kaunti za Nakuru na Kisumu, Kenya**”.

You may now proceed with your Data Collection, Subject to Clearance with Director General, National Commission for Science, Technology and Innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed Supervision Tracking and Progress Report Forms per semester. The Forms are available at the University's Website under Graduate School webpage downloads.

Thank you.

ANNBELL MWANIKI
FOR: DEAN, GRADUATE SCHOOL



C.c. Chairman, Department of Kiswahili.

Supervisors:

1. Prof. Peter Githinji
C/o Idara ya Kiswahili
Kenyatta University

AM/Inn

 REPUBLIC OF KENYA Ref No: 487759	 NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION Date of Issue: 29/July/2021
RESEARCH LICENSE	
	
This is to Certify that Miss. LILIAN MUGUCHE ABUNGA of Kenyatta University, has been licensed to conduct research in Kisumu, Nakuru on the topic: ULINGANISHAJI WA UJIFUNZAJI STADI ZA KISWAHILI KWA WANAFUNZI WENYE ULEMAYU WA MACHO KATIKA SHULE JUMUISIJI KATIKA KAUNTI ZA NAKURU NA KISUMU, KENYA. for the period ending : 29/July/2022.	
License No: NACOSTI/P/21/12055	
Applicant Identification Number 487759	
Director General NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE, TECHNOLOGY & INNOVATION	
Verification QR Code 	
NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.	



OFFICE OF THE PRESIDENT
Ministry of Interior and Coordination of
National Government

Email: ccnakurucounty@yahoo.com
ccnakurucounty@gmail.com

COUNTY COMMISSIONER
 NAKURU COUNTY
 P.O. BOX 81
 NAKURU

When replying please quote:

Ref No. CC. SR. EDU 12/1/2/VOL.V1/32

12th August, 2021

Deputy County Commissioner
NAKURU EAST SUB COUNTY

RE: RESEARCH AUTHORIZATION – MISS LILIAN MUGICHE ABUNGA

The above named from Kenyatta University has been authorized to carry out research on ' **Ulinganishaji wa Ujifunzaji Stadi Za Kiswahili Kwa Wanafunzi Wenye Ulemavu wa Macho Katika Shule Jumuishi Katika Kaunti ya Nakuru**. She will conduct her research in Menengai Primary School in Nakuru East Sub County for a period ending 29th July 2022

Please accord her all the necessary support to facilitate the success of her research.

MWANGI NYAGA
FOR: COUNTY COMMISSIONER
NAKURU COUNTY

MINISTRY OF EDUCATION
STATE DEPARTMENT OF EARLY LEARNING AND BASIC EDUCATION

Telegrams: "EDUCATION",
 Telephone: 051-2216917
 Fax: 051-2217308
 Email: cdenakurucounty@gmail.com
 When replying please quote



COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
 NAKURU COUNTY
 P. O. BOX 259,
 NAKURU.

Ref. NO. CDE/NKU/GEN/4/1/21/VOL.VII

12th August, 2021

TO WHOM IT MAY CONCERN

RE: RESEARCH AUTHORIZATION LILIAN MUGUCHE ABUNGA
NACOSTI/P/21/12327

Reference is made to the above-mentioned permit dated 29th July, 2021.

Authority is hereby granted to the above-named individual to carry out research on:
 "Ulinganishaji wa Ujifunzaji Stadi za Kiswahili kwa Wanafunzi wenye Ulemavu wa
 Macho katika Shule Jumuishi" in Nakuru County, Kenya" for the period ending 29th
 July, 2022.

Kindly accord her necessary assistance.



G.N. Kimani
FOR COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
NAKURU

Copy to:

✓ Kenyatta University



THE PRESIDENCY

MINISTRY OF INTERIOR AND COORDINATION OF NATIONAL GOVERNMENT

Telephone: Kisumu 2022219/Fax: 2022219
Email: ckisumucounty@gmail.com

COUNTY COMMISSIONER
KISUMU COUNTY
P.O. BOX 1912-40100
KISUMU.

Ref: CC/KC/R.ES/1//3/VOL.IV(222)

Date: 16th August, 2021

Deputy County Commissioners
KISUMU COUNTY

RE: RESEARCH AUTHORIZATION – MS LILIAN MUGUCHE ABUNGA

Reference is made to a letter from the National Commission for Science, Technology and Innovation no. NACOSTI/P/21/12055 of 29th July, 2021 on the above underlined subject matter.

The above named is from student from Kenyatta University. She has been authorized to carry out a research on *"Ulinganishaji wa Ujifunzaji Stadi za Kiswahili kwa Wanafunzi wenye Ulemavu wa Macho Katika Shule Jumuishi katika Kaunti za Nakuru na Kisumu"* The research period ends on 29th July, 2022.

Kindly accord her the necessary assistance.

**JOSEPHINE OUKO
COUNTY COMMISSIONER
KISUMU COUNTY.**

Cc: Lilian Muguche Abunga
Kenyatta University

MINISTRY OF EDUCATION
State Department of Early Learning and Basic Education

Telegrams: "schooling", Kisumu
 Telephone: Kisumu 057 - 2024599
 E-mail: countyeducation.kisumu@gmail.com
 When replying please quote:



COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
KISUMU COUNTY
NYANZA PROVINCIAL HEADQUARTERS
3RD FLOOR
P.O. Box 575 - 40100
KISUMU

Ref: CDE/KSM/GA/3/24 VIV/(209)

17th August 2021

The Head teacher
 Joel Omino Primary School

✓ **Thro'**
 The Sub County Director of Education
KISUMU CENTRAL

**RE: AUTHORITY TO CONDUCT RESEARCH AT JOEL OMINO PRIMARY SCHOOL
 BY ABUNGA LILIAN MUGUCHE - NACOSTI 1/P/21/12055**

The above matter refers.

This is to certify that the above named person has been granted permission to conduct research on "ULINGANISHAJI WA UJIFUNZAJI STADI ZA KISWAHILI KWA WANAFUNZI WENYE ULEMAVU WA MACHO KATIKA SHULE JUMUISHI" for the period ending 29th July 2022.

The authority is strictly under the following guidelines: -

1. Covid-19 protocols are strictly observed
2. Normal learning time for the learners is not disrupted
3. No photos or videos are taken without written consent from the parents
4. The researcher reports to the Sub County Director of Educating before proceeding to the school.
5. The Head teacher ensures the researcher works within the confines of the Ministry of Education policies and guidelines in the research process.

NYANKIRA ORINA
FOR: COUNTY DIRECTOR OF EDUCATION
KISUMU COUNTY